# Maswali Na Mishkili Elfu

## (*Alfu Suaal wa Ishkaal*)

## Sehemu ya Kwanza

### Tawhidi ya Mwenyezi Mungu na Sifa Zake Tukufu

**Kimeandikwa na:**
Sheikh 'Ali al-Kuraani al-Aamili

**Kimetarjumiwa na:**
Ustadh Abdallah Mohamed

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 427 - 52 - 9**

Kimeandikwa na:
**Shaikh 'Ali al-Kuraani al-Aamili**

Kimetarjumiwa na:
**Ustadh Abdallah Mohamed**

Kimehaririwa na:
**Hemedi Lubumba Selemani**

Kimepangwa katika Kompyuta na:
**Ukhti Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Novemba, 2008
**Nakala: 1000**

Kimetolewa na kuchapishwa na:
**Al-Itrah Foundation**
S.L.P. - 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info

# YALIYOMO

**Sehemu ya kwanza**

Tawhid ya Mwenyeezi Mungu na sifa zake Tukufu..................................2

**Mas'ala 1**

Dai lao kuwa Mwenyeezi Mungu atakuja aonekana kwa macho..........................................................................................2

**Mas'ala 2**

Kukubali kwa maimamu wao kuwa tawhid yao imetokana na Mayahudi..........................................................................................7

**Mas'ala 3**

Wamemtuhumu Mtume wetu (s.a.w.w) kuwa Padri ndiye aliyemfundisha Tawhidi..........................................................................................17

**Mas'ala 4**

Papa wa hivi karibuni analaumu kule kutakasa kwa Qur'an na anaunga mkono wasemavyo mawahabi juu ya Mwenyeezi Mungu kuwa na umbo..........................................................................................19

**Mas'ala 5**

Imamu wao Ibnu Taymiyya anaamini kuwa Mungu wao ni umbo............21

**Mas'ala 6**

Aina ya ajabu ya ufichaji wwa Imni duniani (Taqiyya). Wanamficha mwabudiwa wao kwa kuogopa waislamu................................................23

**Mas'ala 7**

Je, mnaweza kuyafafanua maneno ya Sheikh wenu Ibnu Uthaymain..........................................................................................25

**Mas'ala 8**

Hadithi ya bedui wanayoitegemea juu ya kumpa umbo Mwenyeezi Mungu..........................................................................................26

**Mas'ala 9**

Hadithi ya Ummu Tufayli inayodai kuwa Mwenyeezi Mungu Mtukufu ni kijana mwenye nywele zilizosokotana......................................................28

**Mas'ala 10**

Vipi mnasema kuwa mola wenu arshi yake inabebwa na wanyama...............................................................................................31

**Mas'ala 11**

Hadith isemayo kwamba Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake na urefu wake ni dhiraa sitini...........................................................32

**Mas'ala 12**

Hadithi zao zinazodai kuwa Arshi ina kelele, mbinja na mlio...................34

**Mas'ala 13**

Je mwawajua wa mwanzo zaidi waliopokea Hadithi za kumshabihisha Mwenyeezi Mungu na kumfanya ana umbo.............................................37

**Mas'ala 14**

Wenye Imani ya kuwa Mungu ana umbo huwakufurisha wenyekuwapinga na huwatisha...............................................................................38

**Mas'ala 15**

Msimamo wenu juu ya Hashawiyya ni upi?.............................................43

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page E

**Mas'ala 16**

Wanaharamisha taawil, na wao wanaifanya, wanakataa kinaya, na wao wanaitumia.....................................................................................47

**Mas'ala 17**

Nini maoni yenu juu ya Hadithi hizi zilizowekwa...................................52

**Mas'ala 18**

Kauli yao kuwa kuna uwili baina ya Mwenyeezi Mungu na sifa zake..56

**Mas'ala 19**

Nini Msimamo wenu juu wanavyuoni wa madhehebu manne na wafuasi wao?.............................................................................................58

**Mas'ala 20**

Kuwatupia shia itikadi yenu ya tashbihi na kumpa Mungu umbo...........58

# UTANGULIZI

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.**

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu. Rehema kamilifu zimfikie bwana wetu na Mtume wetu Muhammad na kizazi chake kitakatifu kitoharifu. Na daima laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya madui zao wote.

Wasiokuwa wafuasi wa madhehebu ya Ahlul-Baiti (a.s.) wametoa baadhi ya mishkeli na utata wao juu ya madhehebu ya haki na wafuasi wake, na wameendelea kurudia hilo ndani ya hotuba zao na vitabu vyao na hatimaye wakayajaza masoko mishkili hiyo na utata huo, wakailundika kwenye tovuti huku wakisambaza vijitabu na mikanda kwa mahujaji na wafanya ziara huko Makka na Madina na kwenye miji mingine ya waisilamu.

Wanavyuoni na wasomi wa Kishia kuanzia wa zamani hadi wa sasa wamejibu mishkili hiyo na utata huo, hivyo tunamuomba Mwenyezi Mungu awalipe malipo bora mno kwa kitendo cha kuwatetea Ahlul-Baiti watoharifu waliodhulumiwa kwa ajili ya kutetea madhehebu yao ya haki.

Maswali haya na mishkili hii ya kielimu tumeiandika ili iwe ni jibu dhidi ya utata wanaouzusha juu yetu, na ili tuweze kuwazindua kuwa kilicho bora zaidi kwao ni kutatua kwanza mishkili na migongano iliyosheheni ndani ya vitabu vyao vya rejea, ambavyo ndio msingi wa fikra za waandishi wao na watafiti wao katika fani ya akida, fiqhi na tafsiri zao, kwani ni bora kutengeneza nyumbani kabla ya kuanza kukosoa kwa jirani. (Pia kabla hujatoa kijiti kwenye jicho la mwenzako kwanza toa boriti kwenye jicho lako).

Ndani ya mishkili hii tumetegemea rejea zao za msingi katika Hadithi, tafsiri, fiqhi, akida na kauli za viongozi wao wakubwa kuanzia wa zamani hadi wa sasa. Ama katika kusanifu milango yake tumetegemea vitabu**:** Mawahabi na Tawhid, uandikwaji wa Qur'an, akida za Kiisilamu na Aya za tukio la Ghadiri na nyinginezo.

Ama mfumo tuliouchagua ni kuhariri suala husika kwa ibara nene inayothibitishwa kwa rejea zao, kisha suala hilo tunalitolea maswali na mishkili, na hapo msomaji na mtafiti anapata wepesi.

Kusudio langu na tawfiki ni kwa Mwenyezi Mungu, na ndiye aongozae kwenye njia sahihi.

**'Ali al-Karaani al-Aamili**
**Shawwal/Mfungo mosi mtukufu 1423 - 2003**

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page H

بسم الله الرحمن الرحيم

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la *Alfu Suaal wa Ishkaal* -sisi tumekiita *Maswali na Mishkili Elfu* kilichoandikwa na Shaikh Ali al-Kuraani al-Aamili na tumekigawa katika mijalada sita, na hili ulilonalo sasa ni jalada la kwanza.

Madhehebu ya Shia Ithnaasharia imekuwa ikishutumiwa na Waislamu wengine shutuma ambazo hazina msingi wala hazimo katika imani na itikadi zake. Shutuma hizi zimekuwa zikirudiwa mara kwa mara licha ya kutolewa majibu madhubuti na yakinifu na wanavyuoni wa zamani na wa sasa.

Kutokana na kasumba hii, mwandishi wa kitabu hiki ameamua kukusanya maswali na mishkili elfu moja kutoka kwenye vitabu vya Kisunni na kutoa hoja kabambe kuzijibu shutuma hizo wanazozuliwa wafuasi wa madhehebu ya Shia. Katika kulitekeleza jukumu hili, mwandishi ametegemea rejea zao za msingi kutoka katika (vitabu vya) hadithi, tafsiri, fikihi na itikadi, na kauli za viongozi wao wakubwa kuanzia wa zamani hadi wa sasa.

Sisi tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu. Katika wakati ambao maadui wa Uislamu na Waislamu wameamua kuungana ili kuubomoa Uislamu, na katika kutekeleza azma yao hii mbinu yao kubwa ni kutumia hitilafu zetu za kimadhehebu; hivyo, tunakitoa katika lugha ya Kiswahili ili wasomaji wetu wa Kiswahili wapate kufaidika na yaliyomo katika safu hii ya masomo na kuongeza ujuzi wao katika masuala ya kidini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Abdallah Mohamed kwa kukubali kuchukua jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam, Tanzania.**

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 1

بسم الله الرحمن الرحيم

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 2



# SEHEMU YA KWANZA:

## TAWHID YA MWENYEZI MUNGU NA SIFA ZAKE TUKUFU

**Mas'ala 1**

### Dai lao kuwa Mwenyezi Mungu atakuja onekana kwa macho!

Wamesema Ahlul-Bait (a.s.) kwamba, hakika Mwenyezi Mungu mtukufu hujulikana kwa akili na kwa moyo, na ni muhali kumwona kwa macho kwa sababu huoni ila kitu cha kimaada ambacho kiko chini ya kanuni za wakati na mahali, na Mwenyezi Mungu mtukufu macho wala mawazo hayamuoni: "Hakuna chochote kama mfano wake, naye ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona."

Imepokewa kutoka kwa Imam Ridha (a.s.) amesema: "Ewe Abu Salt, hakika Mwenyezi Mungu mtukufu hasifiwi kwa mahali, na wala macho na mawazo hayamtambui." (Al-Ihtijaj, Juz. 2, Uk. 190 na Al-kafi, Juz. 1 Uk. 143).

Ama wanaopinga madhehebu ya Ahlul-Bait wamesema kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu atakuja onekana kwa macho huko akhera. Na baadhi yao wamesema, anaonekana kwa macho hata duniani!

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 3



Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira, amesema: "Watu waliuliza, ee Mtume, je tutamuona Mola wetu siku ya Kiyama? Akasema: "Je mnapouangalia mwezi mwandamo ndani ya usiku wa mwezi mpevu mnauona kunapokuwa hakuna mawingu? Wakasema: "La, ewe mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema tena:" mnapoliangalia jua mnaliona kunapokuwa hakuna mawingu? Wakasema: "La, ewe mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: "Basi mtamuona hivyo hivyo." (Sahih Bukhari, Juz. 1 Uk. 195).

Imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Umar, amesema: "Siku moja Mtume (s.a.w.w.) alimtaja Masih Dajjal mbele ya watu, Akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu si chongo, lakini masih Dajjal ni chongo." Yaani Mtume aliwatuliza watu kuwa macho ya Mwenyezi Mungu yote ni mazima! (Sahih Bukhari, Juz. 2 Uk. 141).

Na imenukuliwa kutoka pambizoni mwa sherehe ya Tirmidhi Juz.6 Uk. 188, kutoka kwa Ibnul Arabi: "Kwamba Mwenyezi Mungu hakuteremsha Aya hii, 'Macho hayamuoni' kwa ajili ya kukanusha kuwa haonekani, au kama alivyosema Aisha, kwani Yeye anaonekana duniani na akhera kwa kuwa yajuzu na itatokea."

Na mwanzo wa kudhihiri kwa Hadithi za kuonekana kwa Mungu kwa macho ni kutoka kwa Umar bin Al-Khattab, amesema: "Hakika kiti chake kimeenea mbingu na ardhi na kina mlio kama wa kipando kipya kinapopandwa, kutokana na uzito wake." (Imepokewa na Bazar na wapokezi wake ni wale wa Sahih.) (Majmauz-Zawaid Juz. 1 Uk. 83).

Imepokewa kutoka kwa Abdu bin Hamid, na Ibn Abi Asim katika Sunna, na Bazar, Abi Ya'ala, Ibn Jarir, Abi Sheikh, Tabrani, Ibn Mardawayhi, na Dhayyaul-Muqaddas katika Al-Mukhtar, kutoka kwa Umar: "…kina sauti kama za kipando kipya kinapopandwa kwa uzito wake." (Suyuti katika Durrul Manthur Juz. 1 Uk. 328).

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 4



Inaonekana Umar alichukua kutoka kwa Kaabul Akhbar, ameipokea Ibn Khuzaima katika Tawhdi yake, Uk. 225: “Amesema: “Walikutana Ibn Abbas na Kaab, Akasema Ibnu Abbas: “Sisi Bani Hashim tunadai, au tunasema kuwa Muhammad alimuona Mola wake mara mbili.” Akasema: “Akapiga takbir Kaab mpaka majabali yakamjibu! Akasema: “Mwenyezi Mungu amegawanya kuonekana kwake na kusema kwake baina ya Muhammad na Musa.”

Hii inaonyesha kuwa Kaab alikuwa akidai kuwa kuonekana kwa Mungu na Bani Hashim wakimpinga, akainasibisha hii kwa Bani Hashim akidai kwamba wao wanakubali, na si sahihi!

Katika Tafsiru Tabari, 12:25. kutoka kwa Kaabul Akhbar, alisema kumwambia mtu: “Umeuliza Mola wetu yuko wapi? Yeye yu katika Arshi kuu, ametegemea huku ameweka mguu wake mmoja juu ya mwingine, na masafa ya ardhi hii ambayo wewe uko ni miaka mia tano, kutoka kwenye ardhi hadi nyingine ni mwendo wa miaka mia tano, na unene wake ni miaka mia tano, mpaka kutimia ardhi saba, kisha kutoka ardhini hadi mbinguni ni mwendo wa miaka mia tano, na Mwenyezi Mungu ni mwenye kuitegemea Arshi!”

Ali (a.s.) alimjibu Kaabul Akhbar katika kikao cha Umar na akamkadhibisha, kama Aisha alivyowakadhibisha wale waliodai kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimuona Mola wake. Pia alikadhibisha hilo Ibnu Abbas, Ibnu Masud, na jamii ya maswahaba.

Amepokea Al-Majlisi katika kitabu Biharul Anwar 36:194: kutoka kwa Ibnu Abbas, kwamba siku moja alihudhuria kikao cha Umar bin Khattab, na hapo alikuwapo Kaabul Akhbar, kisha Umar alisema: “Ewe Kaab, wewe umehifadhi Tawrat?’ Akajibu: “Nahifadhi mengi katika hiyo.” Bwana mmoja katika kikao Akasema: “Ewe kiongozi wa waumini! Muulize Mwenyezi Mungu alikuwa wapi kabla hajaumba Arshi yake? Na maji yaliyo chini ya Arshi aliyaumba kutokana na nini?” Umar

akamwambia: "Eee Kaab, je una ujuzi juu ya haya?" Akasema Kaab: "Ndio ee Amirul muuminiina, tunapata katika hekima ya asili kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu alikuwa ni wa kale kabla hajaumba Arshi, na aikuwa juu ya jiwe la Baytu maqdis kwenye hewa, alipotaka kuumba Arshi yake alitema mate yaliyofanya bahari yenye mawimbi na hapo ndio akaumba Arshi yake kutokana na sehemu ya jiwe lililokuwa chini yake na ni la mwisho lililobakia kwa msikiti."

Ibnu Abbas amesema: "Na Ali bin Abi Talib alikuwapo, akamtukuza Mola wake na akasimama na kukung'uta nguo yake. Akamuapia Umar aliporudi kwenye kikao chake, akasema Umar: "Piga mbizi ewe mzamaji, wasema nini ewe Abul Hasan? Najua kuwa ni mwenye kuondoa ghamu" Ali (a.s.) akamgeukia Kaab akasema: "Watu wako wamekosa, na wakapotosha kitabu cha Mwenyezi Mungu na wakaweka maovu ndani yake! Ewe Kaab! Ole wako! Hakika hilo jiwe unalodai halichukui utukufu wake, wala halitoshi utukufu wake, na hewa uliyoitaja haichukui pambizo zake, na lau vingelikuwa jiwe na hewa ni vya kale pamoja naye, basi vingelikuwa na ukale wake, na ametukuka Mwenyezi Mungu mtukufu kuambiwa kuwa ana mahali.

Na wallahi si kama wasemavyo walahidi, wala si kama wanavyodhani wajinga, lakini alikuwapo bila ya mahali kwa namna ambayo fikra hazimfikii, na kusema kwangu, 'alikuwa' ni mshindi wa kuwapo namna yake nayo ni katika aliyofundisha katika ubainifu. Anasema Mwenyezi Mungu: "Amemuumba mwanaadamu na akamfundisha ubainifu." na kusema kwangu 'alikuwa' ni katika aliyonifundisha katika ubainifu ili nitamke hoja na utukufu wake.

Na alikuwa, na ataendelea kuwa, Mola wetu ni mwenye uwezo wa akitakacho na amekizunguka kila kitu, kisha akafanya alivyotaka bila ya fikra iliyozuka, wala shubha iliyomuingilia kwa alichokitaka. Naye mtukufu ameumba nuru aliyoianzisha, kisha akaumba kwayo giza, na alikuwa anaweza kuumba giza bila ya chochote kama alivyoumba nuru bila ya cho-

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 6



chote, kisha akaumba kutoka katika giza nuru na akaumba kutoka katika nuru yakuti uzito wake ni kama wa mbingu saba na ardhi saba, kisha akaizuia yakuti, ikawa ni maji yenye kutetemeka, na bado inatetemeka mpaka siku ya Kiyama. Kisha akaumba Arshi yake kutokana na nuru yake na akaiweka juu ya maji, na Arshi ina ndimi elfu kumi kila ulimi unamsabihi Mwenyezi Mungu kwa lugha elfu kumi hakuna lugha moja inayofanana na nyingine, na Arshi Ilikuwa juu ya maji bila ya pazia (kizuizi) na hiyo ndio kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na Ilikuwa Arshi yake juu ya maji ili awafanyie mtihani."

Ee Kaab, ole wako! Hakika kama ingelikuwa bahari ni mate yake kama usemavyo, basi ingelikuwa kubwa kuliko kuchukuliwa na jiwe la baytul Maqdis au na hewa uliyoiashiria kuwa iliishukia."

Umar akacheka, Akasema: "Hili ndio jambo lenyewe na hivi ndiyo inavyokuwa ilimu, si kama ilimu yako ewe Kaab, siishi katika zama ambazo simuoni Abul Hasan."

## Maswali

**1.** Kwa nini mwafasiri kwa kukubaliana na Umar kuwa mlio wa Arshi ni kutokana na uzito wa Mwenyezi Mungu na kumpa Mungu umbo kwa Kaabul Akhbar, licha ya kauli yake ya wazi Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "hakuna chochote mfano wake, naye ni Msikizi, mwenye kuona."(Shura: 11) na licha ya kukataa Ahlul bait na maswahaba fikra za Kaabul Akhbar?

**2.** Je hamuoni kuwa Hadith ya kumpa Mungu umbo haikuwa maarufu wakati wa Mtume (s.a.w.w.), wala enzi za Abu Bakar, wala haikupokewa ila enzi za Umar kutoka kwa Kaabul Akhbar na jamaa zake kisha wakaichukua wapokezi wa kiBani Umayya, wakaieneza kwa waislamu na kuingiza katika Sahih zao?

**3.** Vipi muifanye dhati ya Mwenyezi Mungu inyenyekee kanuni ya zama na mahali, ambapo Mola (s.w.t.) alikuwapo kabla yazo, yaani hazikuwapo kisha akaziumba?

**4.** Nini maana ya kuharamishwa kutumia mutashabih (maneno yenye maana iliyofichikana) na wajibu wa kufasiri maneno yenye maana iliyofichikana yaliyomo ndani ya Qur'an na Hadith kwa kutumia muhkam (maneno yenye maana iliyo wazi), mna nini nyinyi mwachukua maana iliyofichikana katika Aya za sifa na hamzitafsiri kwa Aya zenye maana iliyo wazi?!

## Mas'ala 2

### Kukubali kwa maimamu wao kuwa tawhid yao imetokana na Mayahudi

Amesema Ibnu Taymiyya katika kitabu 'A-aqlu fi fahmil qur'an' Uk 88: "Inavyojulikana kwa mwenye kuwa na inaya na Qur'an ni kuwa mayahudi hawasemi kuwa Uzayr ni mwana wa Mungu, bali wamesema baadhi yao tu, kama ilivyonukuliwa kwamba alisema Fanhas bin Azura au yeye na mwengine.

Kwa ujumla, wanaosema hivyo katika mayahudi ni wachache, lakini habari hiyo juu ya aina ni kama alivyosema: "Wale waliowaambia watu, hakika watu wamewakusanyikia.." Mwenyezi Mungu (s.w.t.) aliubainisha ukafiri huu ambao waliusema baadhi yao. Kama Ilikuwa ndani ya Tawrat hamna sifa walizozitaja wapingaji kuwa ni kushabihisha na kuwa na umbo, basi zimo za jamii hiyo zinazokanushwa na wapingaji na wanazoziita kuwa ni kushabihisha na kuwa na umbo, bali mna kuthibitisha upande fulani na Mungu kuzungumza kwa sauti, na kumuumba Adam kwa mfano wake na mfano wa mambo haya, ikiwa haya ni katika waliyoyakadhibisha mayahudi na kuyabadilisha, basi ilikuwa kukanusha kwa Mtume (s.a.w.w.) hivyo ni bora zaidi kuliko kutaja yasiyokuwa hayo.

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 8



Vipi! Ilihali yaliyotajwa yanaafikiana na yaliyotajwa katika Tawrat! Utakuta kwa ujumla yaliyotajwa katika kitabu na Hadith katika sifa yanaafikiana na yaliyotajwa katika Tawrat!

Na tulisema hapo awali haya yote kwa kawaida haiwezekani kuwafikiana na yale waliyoyataja bila ya kuwa pamoja, na Musa hakuwa na Muhammad pamoja na Muhammad hakujifunza kutoka kwa Ahlul-kitab, imejulisha hiyo juu ya ukweli wa mitume wakuu wawili, vitabu viwili vikuu."

Ibnu Taymiyya anakusudia kuwa jambo pekee ambalo mayahudi walimtukana Mwenyezi Mungu ni kusema kwao "Uzayru ni mwana wa Mungu." Na hii inamaanisha kuwa yeye alithibitisha sifa zilizobaki za kumfanya Mungu kuwa na umbo, sifa zingine zilizomo katika Tawrat yao.

Ibnu Taymiyya amekuwa ni wa pekee kwa kauli yake juu ya kusihi kwa itikadi za Tawrat. Kwani hakika mwanachuoni mwingine yeyote miongoni mwa waisilamu, hajafahamu kutokana na Qur'an kukanusha umwana wa Uzair kuwa yenyewe imekiri uzushi wa mayahudi katika Tawhid na sifa, na wala hajafahamu kuwa imekiri kuwa Tawrat ya sasa ni sahihi na haijapotoshwa. Naam, hata Bukhari pia amekuwa pekee na Akasema kuwa maneno ya Tawrat ni sahihi kama itakavyokuja.

Ama Muhammad bin Abdul Wahhab, yeye amemfuata imamu wake Ibnu Taymiyya. Akasema katika Hadith ya Haakhaam ambaye walidai kuwa mtu huyo alimfundisha Mtume wetu (s.a.w.w.) Tawhid ya mayahudi.

Katika mwisho wa kitabu chake kiitwacho At-Tawhiid, amesema: "Kuna mas'ala, la kwanza: Ni tafsiri ya kauli yake, 'na ardhi yote nimeikusanya siku ya Kiyama.'

Pili: Hakika ilimu hizi na mfano wake, zilikuwako katika baadhi ya mayahudi waliokuwako wakati wa Mtume, na hawakuzikanusha wala kuz-

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 9



itolea taawili.

Tatu: Yule mwanachuoni alipotaja hivyo kwaMtume (s.a.w.w.) alimsadikisha. Na Qur'an ikashuka pia kulithibitisha hilo.

Nne: Kucheka sana kwa Mtume mbele ya mwanachuoni huyu alipotaja elimu hii kubwa. Tano: Kueleza wazi wazi juu ya mikono miwili, na kwamba mbingu ziko kwenye mkono wa kulia, na ardhi ziko kwenye mkono mwingine.

Sita: Kufafanua juu ya kukuita kaskazini.

Saba: Kuwataja wajuba na wenye kibri hapo.

Nane: Neno lake, ni kama punje ya khardali katika mkono wa mmoja wao.

Tisa: Ukubwa wa kiti kulingana na mbingu.

Kumi: Ukubwa wa Arshi kulingana na kiti.

Kumi na moja: Arshi imebadilisha kiti na maji.

Kumi na mbili: Umbali kati ya mbingu na mbingu.

Kumi na tatu: Umbali kati ya mbingu saba na kiti.

Kumi na nne: Umbali kati ya kiti na maji.

Kumi na tano: Arshi iko juu ya maji.

Kumi na sita: Mungu yuko juu ya Arshi.

Kumi na saba: Umbali kati ya mbingu na ardhi.

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 10



Kumi na nane: Unene wa kila mbingu ni miaka mia tano.

Kumi na tisa: Bahari iliyoko juu ya mbingu, kati ya juu yake na chini yake ni mwendo wa miaka mia tano.

## Maswali

**1.** Kulingana na alivyosema imamu wenu Ibnu Abdul Wahhab katika mas'ala ya pili na ya tatu kwamba ilimu ya Mungu kuwa na umbo, ilikuwa imehifadhiwa kwa mayahudi na yule kiongozi (rabbi) wao alimfundisha mtume (s.a.w.w.), Je Qur'an iliyoshuka Makka haikuwa na maelezo ya Tawhid mpaka Mtume ayapate kutoka kwa myahudi wa Madina?

**2.** Je mnakubaliana na masafa haya aliyoyataja imamu wenu Ibn Abdul Wahhab baina ya mbingu na ardhi na mahali alipo Mwenyezi Mungu, na zinafikia kilomita ngapi?

**3.** Mnajua kuwa Umar bin Khattab aliwakataza waislamu kuiandika Qur'an na Hadith na yeye ndiye aliyekwenda na nakala ya Tawrat iliyotiwa irabu na kumtaka Mtume akubaliane nayo na kuieneza baina ya waislamu, Mtume akamkataza na yeye na jamaa zake akawaita 'Al-mathukina' na kuwahadharisha waislamu nao?

Lakini baada ya Mtume Umar aliendelea kueneza elimu ya kiyahudi iliyokuwa ikimpendeza na aliweza pamoja na Kaabul Akhbar kuleta mapokezi ya ki-israili katika elimu ya kiislamu!

Bukhari naye akamfuata Umar, Akasema: "Tawrat iliyoko ina daraja sahihi kwa matamko yake ni ya kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na ama maana ya kusema mayahudi wamepotosha katika kauli hii ya Mwenyezi Mungu: "Na kwa kutengua kwao ahadi zao, tuliwalaani, na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu, wakiyapotosha maneno kutoka kwenye mahali pake sahihi."

maana yake ni kuwa, wao walikuwa wakifanya taawili, na maana yake sio kuwa waligeuza maneno yake!

Amesema Bukhari katika Sahih yake: Juz. 8 Uk. 216: "Mlango wa kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.):"Bali hiyo ni Qur'an tukufu, imehifadhiwa katika lawh, 'wanapotosha,' yaani hakuna mmoja awezaye kuondosha neno moja katika kitabu cha Mwenyezi Mungu, mtukufu, bali wao wanaleta taawili kinyume na ilivyo taawili yake."

Ama Ibnu Taymiyya amemzidi Bukhari na akachukua itikadi yake juu ya Mwenyezi Mungu kutoka katika Tawrat, na akasema kuwa yote ni sahihi juu ya kuwa Mungu ana umbo, na akakufuru, isipokuwa tu kauli ya kusema kuwa Uzair ni mwana wa Mungu!

Vipi mtakubali madai yake na hali Qur'an imeeleza na waislamu vizazi vyote wamesema kuwa mayahudi na manaswara wameipotosha Tawrat na Injili yao, na kwamba walizo nazo haziaminiki.

Na amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:
"Na kwa kutengua kwao ahadi zao, tuliwalaani, na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu, wakiyapotosha maneno kutoka kwenye mahali pake sahihi. Na wameacha sehemu (kubwa) ya yale waliyokumbushwa. Na utaendelea kupata habari za khiyana zao, isipokuwa wachache miongoni mwao, basi wasamehe na waache. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao mema." (Al-Maida: 13)

Na amesema tena Mwenyezi Mungu mtukufu: "Na mayahudi hawakumuheshimu Mwenyezi Mungu kama inavyotakiwa kumuheshimu, waliposema: "Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote juu ya binaadamu yeyote. Sema 'ni nani aliyeteremsha kitabu alichokileta Musa? Chenye nuru na uongofu kwa watu, mlichokifanya juzuu juzuu, mkadhihirisha na yaliyo mengi mkayaficha. Na mmefundishwa msiyoyajua nyinyi wala baba zenu. Sema 'Mwenyezi Mungu (ndiye aliyeiteremsha hii Qur'an na

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 12



hivyo vingine)’ Kisha waache wacheze katika porojo lao.” (Al-An’aam: 91).

Akasema tena (s.w.t.): “ Hilo ni kwa sababu wao walikuwa wakizipinga Aya za Mwenyezi Mungu na wakiwaua Mitume pasi na haki. Basi haya ni kwa sababu ya kuasi kwao na walikuwa wakipindukia mipaka.” (Baqarah: 61).

Wale wanaokanusha Aya za Mwenyezi Mungu na kuwaua Mitume, basi wao ndio wenye kuweza kupotosha aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu mtukufu, basi vipi tutaamini kilichomo mikononi mwao?

Bali tamaa yao iliwafikisha hata kuipotosha Qur’an tukufu, amesema Mwenyezi Mungu (s.w.t.): “Na hakika katika wao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri maneno yao hayo kuwa ni ya kitabu (cha Mwenyezi Mungu) wala si ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu), na wanasema: “haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu, na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uongo na hali wanajua.” (Ali Imran: 78).

Akasema tena (s.w.t.) : “Je mnatumaini wawaaminini na kulikuwa na kikundi miongoni mwao kikisikiliza maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha kikayapotosha baada ya kuyafahamu na hali wao wanajua?” (Baqara: 75).

4. Mnasemaje juu ya jibu la Ibn Hajar la kumjibu Bukhari na Ibnu Taymiyya?

Amesema katika ‘Fat’hul Bari: Juz. 13 Uk. 436: “Kauli yake kwamba, hakuna mtu anayeondosha neno katika kitabu cha Mungu katika vitabu vyake (s.w.t.) lakini wao wamepotosha taawili yake isiyo kuwa taawili yake sahihi…”

Amesema Sheikh wetu Ibnul Mulaqan katika sherehe yake, kuwa, haya aliyoyasema ni moja kati ya kauli mbili katika tafsiri ya Aya hii, na yenyewe ndio chaguo lake, yaani Bukhari. Watu wetu wengi wamesema wazi wazi kuwa mayahudi na manaswara wamebadilisha Tawrat na Injili, na hata wamefikia kuzitweza karatasi zake, na hii inaenda kinyume na alivyosema Bukhari hapa."

Naye ni kama mwenye kutamka waziwazi kuwa, kauli yake 'yeye si pekee' mpaka mwisho wake ni miongoni mwa maneno ya Bukhari aliyounga mwishoni mwa Tafsiri ya Ibnu Abbas, naye anachukulia kuwa ni maneno ya Ibnu Abbas yaliyobaki katika Tafsiri ya Aya hiyo.

Baadhi ya wafafanuzi wa sasa wamesema: "Wamehitilafiana katika mas'ala haya kwa kauli mbalimbali:
Ya kwanza ni: Ni kuwa wao walibadilisha yote nayo ni kwa muktadha wa kauli ya yule aliyeeleza kufaa kuitweza. Na kauli hiyo ni kuchupa mipaka. Na kuna Aya pamoja na Hadithi nyingi zisemazo kwamba kulibaki vitu vingi bila kubadilishwa. Kati yazo ni kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "…Ambao wanamfuata Mtume asiyesoma wala kuandika ambaye wanampata ameandikwa kwao katika Tawrat na Injil.."

Katika hizo pia ni kile kisa cha kupigwa mawe myahudi, pia kupatikana kwa Aya ya kupiga mawe, na inasisitizwa kwa kauli yake Mwenyezi Mungu: "Sema, hebu leteni Tawrat na muisome ikiwa nyinyi ni wakweli."

Ya pili: Hakika kubadili kumetokea lakini sana na kuna dalili nyingi.

Ya tatu: Kumetokea katika Aya chache, lakini nyingi zimebaki kama zilivyokuwa, kama alivyosema Sheikh Taqiyyu din Ibnu Taymiyya katika kitabu chake 'Ar-raddu sahih a'la man badala diinul masiih'.

Ya nne: Hakika kumetokea kugeuza katika maana na si katika maneno hiyo imetajwa hapa (Yaani hiyo ni kauli ya Bukhari).

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 14



Ibnu Taymmiyya aliulizwa juu ya masuala haya na akajibu katika fatuwa zake: "Wanavyuoni katika hilo wana kauli mbili:Na akatoa hoja ya pili kuwa ndio iliyo na wengi, moja ikiwa ni kauli yake Mwenyezi Mungu: "..Hakuna mwenye kubadilisha maneno yake." Nayo inapingana na kauli nyingine: "na mwenye kuibadilisha baada ya kuisikia, basi madhambi yake ni kwa wale wanaoibadilisha. "Na wala haiwezekani kuainisha uoanishaji wa maana za Aya zilizotajwa kwa kuliletea taawil tamko la Aya inayokataa na kuiletea taawil maana ya Aya inayothibitisha, kwa sababu inaruhusiwa kuiletea hukumu maalumu ile Aya inayokataa, na ile inayothibitisha kuiletea hukumu nyingine itakayojumuisha tamko na maana.

Miongoni mwayo ni kufutwa kwa Tawrat Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini hakuhitilafiani, na ni muhali kuwe na mabadilisho, kisha ifuatie nakili katika mpango mmoja.

Utoaji dalili huu ni wa ajabu kwani kukifaa kuwapo kwa kubadilisha basi imefaa kutokuwapo chenye kubadilishwa, na nakala zilizopo hivi sasa ni zile ambazo zimetulia kwao zikiwa ni zenye kubadilishwa.

Ama kuhusu Tawrat, Bukhtanassar alipoipiga vita Baytul muqaddas na kuwaangamiza Bani israil na kuwararua, aliviondoa vitabu vyao mpaka alpokuja Uzair akawajazia tena hivyo.

Ama kuhusu Injil, Warumi walipoingia kwenye ukristo wafalme na wakubwa wao walikusanya Injili walizokuwa nazo, na kupotosha maana hakukanushwi, bali kupo kwao kwa wingi.

Hakika kuhusu mjadala juu ya je, kama maneno yalipotoshwa au la, ni kuwa katika vitabu hivyo viwili kumepatikana maneno ambayo haifai kabisa maneno haya yawe yametoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.

Ametaja Abu Muhammad Ibnu Hazmi mambo mengi kama haya katika kitabu chake 'Al-faslu fil milal wan-nihal' miongoni mwayo ameyataja

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 15



mwanzoni mwa sehemu ya kwanza katika waraka wa Tawrat ya mayahudi….:..Na kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu wakati Adam alipokula kutoka katika mti, huyu Adam amekuwa ni kama mmoja wetu katika kujua kheri na shari, na wachawi wa Firaun walimfanyia kama vile walivyotumiwa vyura, lakini walishindwa na mbu, na kwamba mabinti wawili wa Nabii Lut baada ya kuangamia kaumu yake, kila mmoja wao alilala na baba yake, baada ya kumlewesha na kila mmoja wao akapata mimba yake! Na mengineyo yasiyokuwa hayo yenye kuchukiza!

Na mahali pengine Ametaja kuwa kubadilishwa kulitokea mpaka ikatokomezwa, kisha Ezra aliyetajwa ndio akaijaza kama ilivyo hivi sasa, kisha akaeleza mambo mbalimbali kutoka kwenye mistari ya Tawrat iliyomo mikononi mwao sasa, na uongo uliomo humo ni dhahiri. Kisha Akasema:"Tumepata habari kwamba kuna baadhi ya waislamu wanakanusha kuwa Tawrat na Injil zilizoko mikononi mwa mayahudi sasa kuwa zimepotoshwa,na sababu inayowapelekea kuamini hivyo ni kule kutokujali kwao sana nasi za Qur'an na Hadith. Imeenea habari kuwa wao wanapotosha maneno kutoka mahali pake, na wanamzulia Mwenyezi Mungu uongo na hali wanajua. Na wanasema haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu, nayo hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu wanachanganya haki na batili na wanificha haki na wao wanajua."

5. Kukubali kwa mayahudi na manaswara kwamba nakala za asili za Tawrat na Injil zimepotea, na kwamba pia zimebadilishwa, na zimeandikwa kwa karne nyingi baada ya mitume yao. Je mnakubali Ibnu Taymiyya awe mwenye uzalendo na Tawrat zaidi ya mayahudi wenyewe?

Katika kitabu 'Muqaranatul adyan' 'Uk. 254' Dkt. Ahmad Shalabi anasema: "Msomi Wall Durant Ametaja maswala haya kwa kifupi, hebu nasi tuchukue sehemu kidogo: "Vitabu hivi viliandikwa vipi, lini, na wapi? Maswali haya yamefanya kuandikwa kwa maelfu ya vitabu lakini yapasa tuhitimishe hapa kwa ibara moja, Wanavyuoni wamekongamana kuwa katika vitabu vya zamani sana ndani ya Tawrat ni Genesis (Mwanzo) baad-

hi viliandikwa kwa yahud na baadhi kwa Israil, kisha kukatokea kuafikiana kati ya kilichoandikwa huku na huko, baada ya kuanguka dola mbili za kiyahudi, na maoni yenye nguvu zaidi ni kuwa kitabu cha Tathniya ni katika maandishi ya Ezra.

Na inaonyesha vitabu vitano vya Tawrat viko namna ambavyo viko hivi sasa kutoka kwenye miaka ya 300 B.C. (Qiswatul hadhaara Juz. 2 Uk. 367-368).

Anasema Mutawali Yusuf Shalabi katika kitabu 'Adhwaaun alal masiihiyya' Uk. 40 : "Vilevile wao wanakubali kwamba nakala ya zamani zaidi ya Injili hii ni ile ya Mathayo, hii Ilikuwa kwa lugha ya kiyunani (kigiriki) na imepotea.

Anasema Jerom Ain: "Mathayo aliandika Injili kwa lugha ya kiebrania naye akiwa katika nchi ya mayahudi kwa ajili ya waumini wa kiyahudi.

**Tarehe ya kuiandika na kuitarjumu**: Wakristo wamehitilafiana sana katika mpamgilio wa tarehe ya kuandikwa na kutarjumiwa Injil ya Mathayo kama ambavyo pia wanahitilafiana juu ya aliyeitarjumu.

1. Mtoto wa Patrick anaonelea kuwa Mathayo aliiandika Injili wakati wa Kaldayo lakini hakutaja hasa mwaka iliyokamilika au wa kuanza kuandikwa kwa Injili hii. Na anasema kuwa aliyeitarjumu ni Yohana.

2. George Zawin (Mlebanon) anasema katika maoni yake: "Mathayo aliandika bishara yake huko Jerusalem mnamo mwaka 39 A.D. (Miladiyya) kwa kuwa yeye aliwaandikia mayahudi waliomuamini Masihi, au aliandikia ikiwa ni majibu kwa mitume, na lugha aliyotumia ni kiebrania, si kigiriki kama alivyotaja Osipedis katika historia yake.

Bwana George Zawin anasema kuwa mwaka iliyoandikwa ni mwaka 39 A.D. na pia ameainisha lugha lakini hakumtaja ni nani aliyeiandika.

3. Dkt. Bost anaonelea kuwa Mathayo aliandika Injili kabla ya kuvunjwa Jerusalem, na aliiandika kwa kigiriki, kwa hili huyu anapingana na wanahistoria wote wa kikristo katika kuafikiana kuwa lugha aliyoandikia Mathayo ilikuwa ni ya kiebrania ama ni ya kisiria.

## Mas'ala 3

**Wamemtuhumu Mtume wetu (s.a.w.w.) kuwa Pdri ndiye aliyemfundisha Tawhid**

Miongoni mwa waliyoyategemea katika kauli yao juu ya kuwa Mungu ana umbo, ni kwamba, Kiongozi wa kiyahudi (rabbi) alikwenda kwa Mtume (s.a.w.w.) na akamwambia kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu ana mwili, mkono na vidole; Mtume naye akamsadiki, na akamchekea.

Katika Sahih Bukhari : Juz. 6 Uk. 33: "Imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Umar, amesema: "Alikuja mmoja katika wanavyuoni wa kiyahudi kwa Mtume (s.a.w.w.), Akasema: "Ewe Muhammd, sisi tunapata kwamba Mwenyezi Mungu anabeba mbingu kwa kidole kimoja, na mti kwa kidole kingine, na maji na mchanga kwa kidole kingine, na viumbe vingine kwa kidole kingine, na husema: "Mimi ni Mfalme." Mtume (s.a.w.w.) akacheka mpaka yakaonekana magego yake kwa kusadikisha maneno ya mwanachuoni huyo!"

Na katika Musnad ya Ahmad: Juz. 1 Uk. 457: "Imepokewa kutoka kwa Abdallah bin Masud, amesema kuwa, alikwenda mwanachuoni mmoja kwa Mtume (s.a.w.w.) Akasema: "Ee Muhammad, au , ee Mtume wa Mwenyezi Mungu, siku ya Kiyama Mwenyezi Mungua atazichukua mbingu katika kidole chake na ardhi katika kidole kingine, milima katika kidole kimoja na mti katika kidole kingine, na maji na mchanga pia katika kidole kingine, ataitikisa kisha aseme, Mimi ndiye Mfalme." Mtume (s.a.w.w.) akacheka mpaka yakaonekana magego yake kwa kuisadikisha kauli ya mwanachuoni huyo."

(Pia hii ameipokea katika sehemu nyingine k.v. Juz. 8 Uk. 174. na 202. Na katika Juz. 6 Uk.33:"Akasema, ee Muhammad, Sisi tunapata Mwenyezi Mungu ataziweka mbingu kwenye kidole………….."Yaani tunapata katika Tawrat au katika vitabu vyetu).

Ameikubali riwaya hii Ibnu Abdul Wahhab na kuitaja mwisho wa kitabu chake alichokiita 'Tawhid', na hata aliiwekea mlango maalum ambao ni mlamgo wa mwisho wa kitabu chake.

## Maswali

**1.** Mungu wenu ana vidole vingapi? Ni vitano au sita? Katika riwaya ya Bukhari ni vitano, katika ya Hambali ni sita, je kwa mahambali kuna kidole kimoja zaidi?

**2.** Kwa nini mmewakhalifu wanavyuoni waliokataa Mtume kuwa amekiri Mungu kuwa na umbo, kwa dalili kuwa alimsomea kauli yake (s.w.t.): "Na hawakumheshimu Mwenyezi Mungu haki ya kumheshimu. Na siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mikononi mwake na mbingi zitakunjwa mikononi mwake. Ameepukana na upungufu na yu juu kabisa kuliko yale wanayomshirikishia." (Zumar: 67). Wamesema: "Ikiwa imesihi Mtume (s.a.w.w.) alicheka, basi alicheka kwa mshangao na kumfanyia maskhara huyo myahudi (rabbi) si kwa kumsadikisha.

Na amesema Nawawi katika Sherehe ya Muslim: Juz. 17 Uk. 30: "Dhahiri ya Hadith ni kuwa Mtume (s.a.w.w.) alimsadiki mwanachuoni huyo kwa kauli yake kuwa Mwenyezi Mungu anazishika mbingu na ardhi na viumbe wengine kwa vidole, kisha akasoma Aya ambayo ndani yake mna ishara ya vile asemavyo."

Amesema Al-Qadhi: "Baadhi ya wasomi wamesema kuwa, kucheka kwa Mtume, kustaajabu na kusoma kwake Aya, hakukuwa ni kusadikisha maneno ya mwanachuoni wa kiyahudi, bali ni kujibu kauli yake na

kuikanusha na kustaajabu kwa namna itikadi yake ilivyo mbaya, kwani madhehebu ya kiyahudi ni kuwa Mungu ana umbo, akafahamu hivyo kutoka kwake. Na kauli yake 'kumsadikisha' hiyo ni maneno ya mpokezi kwa alivyofahamu."

Ibn Hajar amesema katika Faat-hul bari Juz. 13 Uk. 336:"Kucheka kwa Mtume (s.a.w.w.) kutokana na kauli ya mwanachuoni huyo huchukuliwa kuwa ni kuridhia na kukanusha; ama kauli ya mpokezi 'kusadikisha', ni kumdhania.

**3**. Je mnakubali upuuzi huu wa kunasibishwa nasi kwa Mwenyezi Mungu mtukufu: 'akizitingisha na kusema: "Mimi ndiye Mfalme." Na sehemu nyingine: "Mimi Mfalme." Zikikariri kama kwamba anacheza kwa kufurahia uweza wake?

## Mas'ala 4

**Papa wa hivi karibuni analaumu kule kutakasa kwa Qur'an na anaunga mkono wasemavyo mawahabi juu ya Mwenyezi Mungu kuwa na umbo**

John Pope Paul wa pili ametangaza kuwa wakiristo wanasisitiza kuwa Mungu ana umbo, na akaiponda Tawhid na utukuzo katika Qur'an ya waislamu.

Imekuja katika kitabu '**Kupita kwenda kwenye matarajio**' katika mahojiano kati yake na waandishi wa magazeti ya kitalianiVitori Misuori kwa mnasaba wa miaka kumi na mitano ya kutawazwa cheo cha upapa, amesema katika kitabu hicho mashuhuri kilichotolewa katika jarida la Ubalozi wa Lebanon kwa mnasaba wa ziyara ya Papa nchini Lebanon. Papa Amesema: "Atakayeisoma Qur'an na akiangalia maagano yote miwili la kale na jipya, itamdhihirikia wazi kuwa yaliyotokea humo katika wahyi wa Mungu kwa muhtasari, na itakuwa ni muhali asione kutofanana aliyoy-

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 20



asema Mungu kwa dhati yake kupitia kwa manabii zake mwanzo katika agano la kale, kisha kuhitimisha kupitia kwa mwanawe katika agano jipya lenye kujitosheleza ambalo liko wazi katika kufichua dhati ya Mungu, na ambalo linaunda urithi wa thamani wa maagano mawili la kale na jipya. Na hayo yote Uislamu umeyakataa.

Ni kweli hakika, Qur'an inamsifu Mwenyezi Mungu kwa sifa nzuri zaidi zilizopata kusifiwa na ulimi wa mwanaadamu kwa majina yake mema, lakini mwisho wake ni Mola, Mkuu juu ya ulimwengu, mwenye utukufu. Si "Mungu wetu yuko pamoja nasi Emanueli."

## Maswali

**1.** Sisi tunaaafikiana na Papa juu ya kufahamu kwake kuwa Qur'an inamtakasa Mwenyezi Mungu mtukufu, na tunamwambia, Ndio, hakika Mwenyezi Mungu si katika namna ya maumbile kwa sababu yeye ndiye aliyeyaumba..”Hakuna chochote kinachofanana naye, naye ni Msikizi, Mwenye kuona.” Ama nyinyi badala ya kukuza akili zenu katika kumjua Muumbaji wa maumbile, muda na mahali, ambaye Yeye yuko juu yazo, Mtukufu, nyinyi mmemfanya kuwa na mwili ndani ya Nabii Isa (a.s.) na mmemfanya Mwenyezi Mungu kuwa ni kiumbe (mola yu pamoja nanyi na ni kama nyinyi) kulingana na maelezo ya Emanueli.

Je nyinyi mnamwambia Papa kuwa, ngoja ee mwanachuoni, sisi ni kama nyinyi tunaitakidi kuwa Mungu ana umbo la sura ya Adam, naye ni kijana mzuri mwenye nywele zilizosokotana, anavaa sandali mbili za dhahabu.

Je mtamwambia, sisi ni kama nyinyi tumemchukua Mungu wetu kutoka kwa wanavyuoni marejeo yetu katika Tawhid na sifa ni Tawrat nasi tunakubali kila kilichotajwa na Tawrat kwamba yeye amekaa juu ya kiti na pembeni kwake kuna malaika arshi yake inabebwa na malaika wakiwa na umbo la wanyama, ng'ombe, simba, chui na mbuzi mwitu.
Ama Qur'an tutaziawili Aya zake zinazokhalifu hivyo!

**2.** Je hamuoni tofauti kati ya Qur'an ni Bukhari? Na watu wote hata wasiokuwa waislamu wanafahamu kuwa Qur'an inamtukuza Mwenyezi Mungu na kwamba yeye si katika aina za maada na viumbe, ambapo nyinyi mnafahamu katika Bukhari kuna kufananisha na kuwa na umbo na kwa sababu yake mnatoa hoja za kushikamana na Aya zinazoshabihiana katika Qur'an na kuacha zile zilizo wazi.

## Mas'ala 5

**Imam wao Ibnu Taymiyya anaamini kuwa Mungu wao ni umbo!**

Amesema katika kitabu 'Talbisil jahamiyya' Uk. 619: "Baadhi yao wamesema: "Mwenyezi Mungu mtukufu amesema:" Baada yake kaumu ya Musa wakachukua (alipoondoka) mapambo yao, wakatengeneza ndama mwenye mwili anayetoa sauti. Je hawaoni kwamba ndama huyo hawasemeshi wala hawaongozi njia na hali walikuwa wamepotea?"

Hakika Mwenyezi Mungu amemtukana yule aliyemfanya Mungu kuwa na mwili na mwili ni umbo basi Mwenyezi Mungu anakuwa amemtukana mwenye kumfanya Mungu Yeye kuwa ni umbo.

Inasemwa kuwa hii ni batili kwa njia nyingi: Moja ni: Hii inajulisha kuwa hawezi kuwa mwili na hawezi kuwa umbo, na umbo ndani ya istilahi ni sifa pana inayojumuisha zaidi ya mwili!"

Na Akasema katika 'Minhajis Sunna' Juz. 2 Uk. 563: "Huyu mtunzi wa kishia-akimkusudia Allama Hilli katika kitabu chake, 'Minhajul karama'-ametegemea njia ya Muutazila na wanaowafuata kwamba katika kumtakasa Mwenyezi Mungu na kasoro ni kukanusha kuwa Yeye ni umbo na inavyojulikana, njia hii haikutajwa katika Qur'an wala katika Sunna (Hadith) wala kupokewa kutoka kwa mmoja wa masalafi wema hivyo imejulikana kuwa haina asili katika sharia!"

## Maswali

1. Je kuna tofauti gani kati ya kusema kuwa Mwenyezi Mungu mtukufu ni umbo au mwili? Zote hizo ni katika maumbile zinahitaji mahali na wakati, na Mwenyezi Mungu anasema:

"Hakuna chochote kinachofanana naye, naye ni Msikizi, Mwenye kuona." (Shuraa: 1)

Na kutokana na kauli ya sheikh wenu Ibnu Taymiyya: "Hii inajulisha kuwa hawezi kuwa mwili na si hawezi kuwa umbo" Mwenyezi Mungu mtukufu anakuwa ni umbo na hasadikiwi kuwa "Yeye hakuna kinachofanana naye."

2. Sisi hatusemi kuwa Mwenyezi Mungu ni umbo, bali tunasema si kama vitu vingine tumtoe katika mipaka miwili, wa kutotaka kumjua na kumfananisha kama walivyotuamrisha maimamu wetu (a.s.), na madam Sheikh wenu asema kwamba Mungu ni umbo, basi kwa nini alaumiwe Hisham bin Al-Hakam kwa kauli iliyonasibishwa kwake kuwa Mungu ni umbo lakini si kama maumbo mengine?

Hebu angalieni aliyoyasema Sheikh wenu, Nasir Al-Faqari katika kitabu chake 'Usulu madh-habus shial imamiyya': Juz. 1 Uk. 529:"Amepanga Sheikhul Islam Ibnu Taymiyya, yule wa mwanzo kuleta neno ovu zaidi katika hao Akasema: "Na mtu wa kwanza aliyejulikana katika Uislamu kuwa alisema Mungu ni mwili, ni Hisham bin Al-Hakam. (Tazama: minhajus sunna Juz. 1 Uk. 20).

Ikiwa neno la kusema kuwa Mwenyezi Mungu ni mwili kuwa ni kosa kwa nini Ibnu Taymiya anaizusha? Na kama hilo ni sahihi kwa nini basi alilolisema Hisham bin Al-Hakam alilifanya ni kufuru na lake yeye ni imani?

## Mas’ala 6

**Aina ya ajabu ya ufichaji wa imani duniani (taqiyya). Wanamficha mwabudiwa wao kwa kuogopa waislamu!**

Mawahabi wanawalaumu Shia kuwa wao wanatumia njia ya ufichaji wa imani, ilihali ambapo taqiyya ni njia ya kibinadamu ya kimaumbile, na ni hukmu aliyoiweka Mwenyezi Mungu katika kitabu chake kwa waislamu ili watu waijikinge na dhalimu wakati wanapohofia kupoteza roho na mali!

Na mawahabi wao wenyewe wanautumia ufichaji wa imani katika maisha yao ya kila siku, bali wanatumia aina mbaya zaidi ya ufichaji wa imani kwa waislamu, nao ni ufichaji wa imani kuhusu Mungu anayeabudiwa ‘mwenye mwili’ ambaye wao wanamwabudu! Na wanamficha! Kwamba Yeye ni kijana, mwenye nywele nyingi, miguu yake iko kwenye manyasi, amevaa sandali mbili za dhahabu na usoni kwake ana firashi ya dhahabu!

Amepokea Daru Qutni katika kitabu chake ‘Ruuyatul laah’ Uk. 190: “Amesema: “Ametuhadithia Muhammad bin Ismail Al-farisi, ametuhadithia Abu Zar’a Damishqi, ametuhadithia Ahmad bin Swaleh, kwamba Said bin Abi Hilal alimwambia kutoka kwa Marwan bin Uthman, amemwambia kutoka kwa Amara bin Amir, kutoka kwa Ummu Tufayli mwanamke wa Ubayya bin Ka’ab kwamba mwanamke huyo alimsikia Mtume (s.a.w.w.) akitaja kuwa: “Alimuona Mola wake mtukufu usingizini katika suru ya kijana, mwenye nywele nyingi, miguu yake iko kwenye manyasi, amevaa sandali mbili za dhahabu na usoni kwake ana firashi ya dhahabu!”Na ameikubali Imamu wao Ibu Taymiyya katika mkusanyiko wa fatuwa zake Juz. 3 Uk. 336, na 386 na zinginezo.

Na amesema Imam wao Dhahabi katika ‘siir A’alaamihi’ Juz. 10 Uk. 602: “Ama habari ya Ummu Tufayli, aliipokea Muhammad bin Ismail Tirmidhi na wengineo, kisha akaisahihisha Dhahabi Hadith hii na akakanusha awe amelala Akasema: “Ali (r.a.) amesema: “Waliwahadithia watu yale waliy-

oyajua, na wakaacha waliyoyakanusha." Na imesihi kuwa Abu Huraira alificha Hadith nyingi ambazo mwislamu hazihitajii katika dini yake na alikuwa akisema:"lau ningezitoa kwenu basi ningekatwa koo hii." Na hii si chochoe katika mlango wa kuficha elimu, hakika elimu ipasayo ni lazima kuitoa na kuieneza na inapasa umma kuihifadhi na elimu ambayo ni katika fadhila za amali, inayosihi isnadi yake, kunukuu kwake huwa kumeainishwa na kuenezwa kwake husisitizwa, na yapasa kwa umma kuinakili. Na elimu ya halali haipasi kuitoa na wala haifai kuingia ndani yake ila wanavyuoni maalum."

Na kusudio la elimu ya halali yaani ni iliyokatazwa, hii inatokana na kanuni ya kukiita kitu kwa kinyume chake, hivyo yapasa ifichwe ila kwa wanavyuoni maalum! Ni kama ile elimu wanayoidhibiti mayahudi na manaswara makasisi wa Ikloros yaani makadinali wakubwa na marabbi!

Ameweka kiongozi wa mawahabi katika kitabu cha Tawhid yake mlango wenye kichwa cha habari: 'Mlango wa mwenye kukanusha kitu katika majina na sifa.' Akisema kuwa, kuamini sifa zote za Mwenyezi Mungu mtukufu ni wajibu na kukanusha sifa yoyote ile ni ukafiri; na kwamba idadi ya sifa za Mwenyezi Mungu kwenye madhehebu yake inalazimu Mungu kuwa na umbo, kama ulivyoona katika ufafanuzi kwenye Hadithi ya rabbi, hivyo alizungumza wajibu wa kuficha, na mtu kama Dhahabi akatoa ushahidi kupitia riwaya mbili kutoka kwa Ali (a.s.) na Ibn Abbas, ili athibitishe kufaa kuificha elimu hii bila kujali kuwa riwaya mbili hizo hazina uhusiano wowote na maudhui!

## Maswali

**1.** Kwa nini mawahabi wanaogopa kusema wazi kwa waislamu kuwa wanayemwabudu ni kijana mwenye nywele zilizosokotana, ana mng'aro kwenye paji lake, anavaa sandali mbili za dhahabu…mpaka mwisho wa alivyo?

**2.** Kwa nini wanavyuoni wao hawatoi fatuwa ya kupendekeza litengenezwe sanamu la wanayemwabudu ili wawalee watoto wao katika kumjua, na waliweke majumbani na ndani ya magari yao ili wamtaje sana?

**3.** Je kuna tofauti ya kimsingi kati ya wao kuabudu kwao kijana mwenye nywele zilizosokotana na kati ya mayahudi wanaomwanudu mzee na masikh wanaoabudu masanamu yao mbali mbali?

**4.** Vipi wanadai wao ni watu wa Tawhid na kwamba wao wameinyanyua bendera ya Tawhid na hali wanaabudu kijana aliye na sura ya Adam mwenye nywele zilizosokotana?

**5.** Vipi wanatoa fatuwa kuwakufurisha waislamu na kuwatuhumu kuwa wanamshirikisha Mwenyezi Mungu kwa sababu wanatawasali kwa kupitia Mtume Wake, na huku wao wakiabudu sanamu lililoumbwa wakidai kuwa ni Mungu Muumba? (Utakasifu ni wa Mwenyezi Mungu, ametukuka na wanayomshirikisha).

## Mas’ala 7

**Je mnaweza kuyafafanua maneno ya Sheikh wenu Ibnu Uthaymain?**

Amesema katika Sherehe ya Al-Aqidatul wasita ya Ibn Taymiyya Uk. 250: “Ama kuhusu umbo tunasema hivi: Mnakusudia nini kuhusu umbo? Mnakusudia ni umbo lililoshehenezwa mifupa na nyama, ngozi na vinginevyo? Hii ni batili na ni kinyume na Allah, kwani yeye hakuna mfano wake kitu chochote, naye ni Msikizi, Mwenye kuona. Au mnakusudia umbo lililosimama lenyewe likiwa na sifa ya ilivyokuwa navyo?

Hii kweli ndio kwa ilivyo maana, lakini hatusemi kwa kukanusha au kuthibiisha.”

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 26



## Maswali

**1.** Ibn Uthaymain anakanusha kuwa Mungu hawi na umbo katika aina ya maumbo yetu lenye nyama na mifupa, mpaka hapa inawezekana kusemwa kuwa kusudio lake ni kuwa Mwenyezi Mungu ni kitu lakini si kama vitu vingine, na hii inaoana na kauli yake (s.w.t.): "Hakuna kitu chochote kinachofanana naye, naye ni Msikizi, Mwenye kuona." Lakini hapana budi hapa kuongeza kuwa kutokana na sifa ya maumbile aliyompa Mwenyezi Mungu yeye anasema ni sahihi kuwa Adam ana sura ya Mwenyezi Mungu, na ana mkono wenye vidole vitano kama inavyosema riwaya ya Bukhari au vidole sita kama inavyosema riwaya ya Ahmad, na kwamba ana viungo vingine kama wanavyoitakidi! Hii inahukumu kuwa awe na umbo la kimaada, je atasema kuwa Mungu umbo lake si kama la nyama na mifupa bali ni maada nyingine?

Na baada ya kuthibitisha umbo kimaana basi yafaa nini kutaja kuwa ana umbo au kukanusha, kama alivyosema: "Lakini hatusemi kwa kukanusha au kuthibiisha."

Je hii si katika ujanja wa kimaneno anayoyatumia Ibnu Taymiyya na wanafunzi wake?

## Mas'ala 8

### Hadithi ya bedui wanayoitegemea juu ya kumpa umbo Mwenyezi Mungu

Ibnu Taymiyya amedai kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t.) yuko katika upande fulani na anathibitisha kwa Hadith ya Abi Razin Al-Uqaiyli, kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu kabla ya kuumba viumbe alikuwa katika mawingu mazito, chini yake kuna hewa na juu yake kuna hewa.

Amepokea Ahmad Juz. 4 Uk. 11:"Kutoka kwa Wakii, kutoka kwa ami yake Ibnu Razin, amesema: "Nilisema, ee Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mola wetu alikuwa wapi kabla hajaumba viumbe vyake? Akasema:" Alikuwa katika mawingu mazito, chini yake kuna hewa na juu yake kuna hewa, kisha akaiumba Arshi yake juu ya maji." (Imepokewa katika, Juz. 4 Uk. 12, na Ibnu Maja, Juz. 1 Uk. 64/181. Tirmidhi: Juz. 4 Uk. 351/5109. Na Tabrani katika Mu'ujamul kabir Juz. 19 Uk. 207 na wengineo).

Wanavyuoni wa elimu ya uadilifu na kasoro za wapokezi wameikataa Hadith hii lakini Ibnu Taymiyya bado ameing'ang'ania na akaitolea ushahidi katika vitabu vyake zaidi ya mara thelathini!

Amesema katika kitabu chake 'Al-Istiqama Uk. 126: "Akamwambia Abu Razin Al-Uqayli: "Mola wetu alikuwa wapi kabla hajaumba mbingu na ardhi?" Akasema: "Alikuwa katika mawingu mazito chini yake kuna hewa na juu yake kuna hewa, kisha akaumba Arshi Yake juu ya maji" anayekanusha alikuwa wapi basi yahitaji atoe dalili ya kupinga dalili hiyo."

Na amesema katika Taawil mukhtalifil hadith'Uk. 206: "Nasi twasema kuwa Hadith hii ya Abi Razin ina kuhitalifiana, kuna iliyokuja kwa namna nyingine isiyo hii kwa maneno mengine machafu." Al-albani alilazimika kuifanya 'dhaifu' katika kitabu 'Dhaif Ibnu Maja' Uk. 17 namba 181, lakini wakati huo huo amendika kuiamini kwake hata asimuudhi yule anayemtukuza Ibnu Taymiyya!

Amesema Al-AlBani katika kitabu ' Dhilalul-Jannah Uk. 612. na Mukhtasarul u'luwwi Uk. 250/193: "Ni dhaifu." kisha katengua maneno hayo pambizoni mwa kitabu chake' Akasema: Neno 'Al-a'amau' yaani ni mawingu, wamesema wanavyuoni, hii ni katika hadithi za sifa tunaiamini bila ya taawili wala tashbihi na undani wake tunamwachia mjuzi wake."

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 28



## Maswali

**1.** Vipi mnapokea dini yenu na asili ya itikadi yenu katika Tawhid kutoka kwa Abi Razin Al-Uqayli bedui ambaye wanavyuoni wamemfanya kuwa ni dhaifu wa upokezi na wakashuhudia kwa kutomjua?

**2.** Vipi mnaamini Hadithi ya bedui huyu na ilihali yenyewe inalizimu hewa, mbingu, mahali na wakati vyote hivyo viwe pamoja na Mwenyezi Mungu kabla ya kuumba viumbe?

Ni maana yake ni kuwapo miungu mine ya kale pamoja na Mwenyezi Mungu au kabla yake Yeye..Mungu apishie mbali!
Je mmeongeza juu ya kauli ya wakristo ya utatu, nanyi mkasema utano?

**3.** Je mmeona namna gani alivyoifanya dhaifu Al-Bani hadith ya Abi razin na kuiporomosha, kisha akanakili kauli ya mmoja wao katika kumuamini kama kwamba amemridhia:"Basi tunaamini bila ya taawili wala tashbihi!"

## Mas'ala 9

**Hadithi ya Ummu Tufayli inayodai kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kijana mwenye nywele zilizosokotana!**

Wamepokea kwamba Mtume (s.a.w.w.) alimuona Mola wake akiwa ni kijana mwenye nywele nyingi (Mungu apishie mbali!) akiwa amevaa sandali mbili za dhahabu, amesimama kwenye ardhi ya rangi ya kijani kibichi, na maimamu wao wote wamesema kuwa hii ni sahih!

Amesema Dhahabi katika kitabu Sira Juz. 10 Uk. 602: "Ama Hadithi ya Tufayli ameipokea Muhammad bin Ismail Tirmidhi na wengineo: Ametuhadithia Naim, ametuhadithia Ibnu Wahab, ametuambia Amru ibnul Harith, kutoka kwa Said bin Hilal kwamba Marwan bin Uthman amemuha-

dithia, kutoka kwa Ammara bin Amir, kutoka kwa Ummu Tufayl mwanamke wa Abi Kaab: "Nimemsikia Mtume (s.a.w.w.) akitaja kuwa yeye amemuona Mola wake katika sura kadha." Hii ni Hadithi yenye kukanushwa sana. Nasai amesema: "Kwani Marwan bin Uthman ni nani mpaka asadikishwe juu ya Mungu?"

Naim hakuwa pekee katika hili, pia amepokea Ahmad bin Swaleh Al-Misri Al-Hafidh.

Na Ahmad bin Isa Tastari, na Ahmad bin Abdurahman bin Wahbi, kutoka kwa Bin Wahab amesema Abu Zara' Nasri: "Wapokezi wake wanajulikana."

Dhahabi amesema: "Nimesema, bila shaka amehadithia Ibnu Abi Wahbi na sheikh wake na Ibnu Abi Hilal, na wao wanajulikana ni waadilifu. Ama huyu Marwani, ni yupi huyu Marwan? Huyu ni mjukuu wa Abi said bin Almaali Al-Answari, na Sheikh wake ni Ammara bin Amir bin Amru bin Hazmi Al-Answari, kama tukijuzisha kuwa Mtume alisema hivyo, basi yeye anajua zaidi aliyoyasema, na kuona kwake usingizini, ni maelezo ambayo Mtume (s.a.w.w.) hakuyataja, wala sisi hatupendi kuyataja, hivyo tuyachukulie kwa hisia za dhahiri tu, lakini twajilinda na Mwenyezi Mungu tusizame ndani katika kuliamini hilo, kwani baadhi ya waheshimiwa wamesema: "Inapotosha Hadithi." Na huo ni mtazamo duni mno. Na Ali (r.a) amesema: "Wahadithieni watu yale wanayoyajua na yaacheni wanayoyakanusha."

Na imesihi kuwa Abu Huraira alificha Hadithi nyingi ambazo Mwislamu hazihitajii katika dini yake, na alikuwa akisema: "Lau ningelizitoa kwenu basi koo hii ingelikatwa." Na hii si chochoe katika mlango wa kuficha elimu, hakika elimu ipasayo ni lazima kuitoa na kuieneza na inapasa umma kuihifadhi na elimu ambayo ni katika fadhila za amali, inayosihi isnadi yake, kunukuu kwake huwa kumeainishwa na kuenezwa kwake husisitizwa, na yapasa kwa umma kuinakili. Na elimu ya halali haipasi kuitoa na

wala haifai kuingia ndani yake ila wanavyuoni maalum." (Mwisho wa maneno ya Dhahabi).

Na kusudio la elimu ya halali yaani ni iliyokatazwa, hii inatokana na kanuni ya kukiita kitu kwa kinyume chake, na amenakili maneno yake hasa takribani imamu wa mawahabi ambapo ameweka mlango mwisho wa kitabu chake cha Tawhid, unaoitwa: Mlango wa anayekanusha kitu katika majina na sifa. Na anakusudia kuwa kuamini sifa zote za Mwenyezi Mungu ni wajibu na kukanusha yoyote ile ni ukafiri, na kwakuwa idadi ya sifa za Mwenyezi Mungu mtukufu juu ya madhehebu yake zinalazimu Mungu awe na umbo, kwa hivyo amenakili maneno ya Dhahabi kuhusu wajibu wa kuficha elimu hiyo ila kwa watu wake maalum tu!

Albani amekubaliana na usahihi wa marejeo ya Hadithi hiyo ikiwa ni kufafanua Hadithi ya Ibnu Abi Asim namba, 471, na imekuja kwamba yeye alimsikia Mtume (s.a.w.w.) akitaja kuwa alimwona Mola wake usingizini: "Akiwa katika sura nzuri, kijana, miguu yake ikiwa juu ya manyasi akiwa amevaa sandali mbili za dhahabu, na usoni kwake ana firashi ya dhahabu."

## Maswali

**1.** Maadamu Hadithi ya Ummu Tufayl ni miongoni mwa Hadithi zenye maana yenye mgongano ambazo watu wamehitilafiana juu ya usahihi wake, kwa nini basi mshikamane nayo na mkaziacha Hadithi za kutakasa zenye kuafikiwa usahihi wake?

**2.** Maadamu mnawajibisha kuficha elimu ya kumjua Mungu mtukufu, je mnasema kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akificha sifa muhimu sana ya Mola wake kwa watu wote? Na ni nini hukmu ya mwahabi anayesema kuwa mimi sitaki kuficha sifa za Mola wangu bali nataka niwaambie wanangu na niwafanyie sanamu nyumbani kwangu mpaka wamjue mola wao tangu wakiwa wadogo?

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 31



**3.** Imetajwa kuwa katika sifa za Mola wenu kuwa alikuwa na nywele za kusokotana, na ndefu za singasinga, je mlishamwona mtu mwenye nywele zilizosokotana na ndefu za singasinga?

**Mas'ala 10**

**Vipi mnasema kuwa Mola wenu Arshi Yake inabebwa na wanyama?**

Katika mwisho wa kitabu chake 'Tawhid' amesema Imam wa mawahabi Muhammad bin Abdul Wahhab kuwa ni sahihi hadithi ya mbuzi mwitu wanaoibeba Arshi ya Mwenyezi Mungu mtukufu! Na akainasibisha kwa Mtume (s.a.w.w.) kuwa amesema: "Mnaona wangapi kati yenu na kati ya mbingu?" Wakajibu: "Hatujui." Akasema: "Hakika baina yenu na baina yao ni miaka, ima ni sabini na moja au na mbili au na tatu, (kama kwamba ni shaka inatoka kwa Mtume kwa kuwa Ibnu Abdul Wahhab hakutaja kuwa shaka yatokana na mpokezi) na mbingu juu yake hivyo hivyo mpaka zikahesabiwa mbingu saba, kisha juu ya mbingu ya saba kuna bahari ambayo kati ya juu yake na chini yake ni kama ilivyo kati ya mbingu na mbingu, kisha juu ya hivyo kuna mbuzi mwitu wanane, ambao kati ya kwato zao na magoti yao ni kama kutoka mbingu moja hadi mbingu nyingine, kisha migongoni mwao kuna Arshi kati ya juu yake na chini yake ni kama vile baina ya mbingu moja hadi nyingine, kisha Mwenyezi Mungu yuko juu ya hiyo…Ametukuka Mola!

## Maswali

**1.** Mmekubali riwaya ya mbuzi mwitu wanaobeba Arshi, je mnazikubali riwaya zenu zisemazo kuwa simba, ng'ombe wanashirikiana na mbuzi mwitu katika kuibeba Arshi ya Mola wenu?

**2.** Je mwaharamisha nyama za mbuzi mwitu kwa sababu ni mnyama mwenye kutukuzwa kwa ajili ya kubeba Arshi ya Mola wenu?

**3.** Kwa mujibu wa Hadithi ya mnayedai kuwa ni Imamu wenu ni kwamba umbali wa kutoka aridhini hadi kwa Mola wenu unakuwa ni karibuni kilometa laki moja na elfu hamsini! Kwa sababu huo ni umbali wa mbingu kumi, na kuifikia mbingu moja kwa kutembe kwa miguu kunahitaji miaka sabini na tatu, na uwiano wa wa kutembea kwa mwanadamu mwaka mzima ni kilometa elfu kumi na tano, kwa uwiano wa kutembea karibuni kilometa arubaini kwa siku, hivyo eneo alilopo Mola wenu ni kati ya ardhi na mwezi! Je, mnakubali hilo?!!

**4.** Je hamumhofii Mola wenu na ndege za angani wanazozirusha?

## Mas'ala 11

### Hadith isemayo kwamba Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake na urefu wake ni dhiraa sitini

Asili ya Hadithi hii kama alivyoibainisha Imam Ridha (a.s.) ni kwamba, Mtume (s.a.w.w.) alimwona mtu akimtukana rafiki yake na akisema: "Mungu aufanye mbaya uso wako!" Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Usimwambie hivyo-Mungu aufanye mbaya uso wake, kwani Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake." Yaani sura zinazotukanwa, basi usiilaani sura ya nduguyo ambayo Mungu ameichagua kwa baba yetu Adam na wanawe.

Lakini wao wameipotosha wakasema kama walivyosema mayahudi kwamba Mungu ana sura ya mwanaadamu na kwamba Mtume (s.a.w.w.) alisema: "Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake na urefu wake ni dhiraa sitini.!

Katika kitabu 'Fatawa Ibnu Baaz Juz. 4 Uk. 368 Hadithi Na. 2331: " Swali: Kutoka kwa Abu Huraira, kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake, dhiraa sitini." Je, Hadithi hii ni sahihi?

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 33



Jibu: Nassi ya Hadithi: “ Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake, dhiraa sitini kisha akasema: “Nenda ukawasalimie kundi lile, nalo ni kundi la malaika wamekaa, na usikilize, watakavyokuamkia basi hayo ndiyo maamkuzi yako na ya kizazi chako; akaenda, na akasema: “ As-salam a’laykum.” Wakasema: “As-slaamu a’layka warahmatul laahi, wakamzidishia ‘warahmayul laahi’na kila atakayeingia Peponi atakuwa na sura ya Adam urefu wake ni dhiraa sitini.” Bado umbile linaendelea kupungua hadi hivi sasa.

(Ameipokea Ahmad, Bukhari na Muslim, nayo ni Hadithi sahihi wala matini yake haina ajabu, kwani ina maana mbili: Ya kwanza, Mwenyezi Mungu hakumuumba Adam mdogo mfupi, kama watoto wadogo wa kizazi chake kisha akakua na kurefuka mpaka akafikia dhiraa sitini, bali alimjaalia urefu ileile siku aliyozaliwa akiwa katika sura Yake urefu wake ukiwa dhiraa sitini.

Ya pili, dhamiri ya kauli yake, a’laa suuratihi’ عَلَى صُوْرَتِهِ kwa sura yake yarudi kwa Mwenyezi Mungu kwa dalili iliyokuja katika riwaya nyingine sahihi kwa neno ; a’laa suratir rahman عَلَى صُوْرَةِ الرَّحْمٰن nayo ndiyo dhahiri ya mtiririko wa maneno wala hilo halilazimu tashbihi, kwani Mwenyezi Mungu amejiita kwa majina aliyowaita kwayo viumbe wake na akajitolea wasifu kwa sifa alizovisifu viumbe vyake na hilo halilazimu tashbihi na pia sura, wala kuthibitisha huko hakulazimu Mungu kufanana na viumbe vyake kwa sababu kushirikiana katika jina na katika maana hakulazimu tashbihi katika yanayomuhusu kila mmoja kati yao. Kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezi Mungu: “Hakuna kitu chochote anachofanana nacho naye ni Mwenye kuona, Mwenye kusikia.”

## Maswali

**1.** Imam wenu amekiri kuwa akida haifai kujengwa kutokana na habari ya wapokezi wachache, vipi sasa anajipinga mwenyewe na kuwajengea itikadi yenu juu ya dhati ya Mola kutokana na habari ya mpokezi mmoja

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 34



anayetuhumiwa katika upokezi wake na ndiyo miongoni mwa akida kubwa zaidi?

Ibnu Taymiyya amesema katika Minhaj yake Juz. 2 Uk. 133: “Pili: Hii ni katika Hadithi zenye wapokezi wachache, inakuwaje sasa asili ya dini, asili ambayo haisihi imani ila kwayo inathibitishwa kwa Hadithi hiyo?”

Ibnul Jawzi ameweka mlango wa kuthibitisha hilo katika kitabu chake ‘Daf’u shib-hi tashbiihi’ Uk. 28 akasema: “Mlango wa tatu, kuthibitisha kwamba Hadithi ya wapokezi wachache yafidisha dhana wala haifidishi elimu kwa masalafi na maimamu wa Hadithi na kwayo haijengwi misingi ya dini.”

**2.** Kwa nini mkachukua maelezo ya Hadithi hii yenye mkanganyo na hamkuchukua iliyo wazi, na mmeona maneno ya maimamu wa madhehebu katika ufafanuzi wake!

**3.** Maadamu Ibn Baaz anasema Adam ana sura ya Mwenyezi Mungu, Naye ana sura ya Adam, na kwamba hii si tashbihi kabisa, je mnakubali tukisema, fulani ana sura ya Adam na Adam ana sura ya huyo fulani? Naye hafanani na Adam kamwe! Na hatimaye tukanushe kuwa hafanani na wana wa Adam? Je Kadhi wenu atakubali akiambiwa kuwa, sura hii ni sura ya mhalifu lakini hafanani naye kamwe?

## Mas’ala 12

### Hadithi zao zinazodai kuwa Arshi ina kelele, mbinja na mlio

Wamepokea kutoka kwa Umar na wengineo kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu hukaa juu ya Arshi Yake, nayo ina kelele na mbinja na mlio (Ametakasika na ametukuka na wanayomsifia).

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 35



Katika kitabu 'Majmauz Zawaid Juz. 1 Uk. 82: "Kutoka kwa Umar kwamba, mwanamke alikwenda kwa Mtume (s.a.w.w.) akasema: "Niombee Mungu niingie Peponi, Mtume akamtukuza Mola mtukufu na akasema: "Hakika kiti chake kimeenea mbingu na ardhi, nacho kina mlio kama wa kipando kipya kinapopandwa kwa uzito wake."

Haitham akasema: "Ameipokea Hadithi hii Al-Bazaz na wapokezi wake ni sahihi."

## Maswali

**1.** Vipi mtapokea kinachopingana na akili na Qur'an hata kama kimepokewa na wapokezi wakweli?

**2.** Je zinakubali akili zenu kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu Muumba wa kila kitu na asiye na mfano na chochote kipatikane kitu cha kimaada chenye uzani na uzito?

**3.** Nini maoni yenu juu ya tuliyopokea kwenye kitabu Al-kafi Juz. 1 Uk. 130:"Kutoka kwa Swafwan bin Yahya, amesema: "Aliniuliza Abu Qurrat nimuingize kwa Abul Hasan Ridhaa, nikamuombea idhini, nikaruhusiwa. Akaingia, akamuuliza juu ya halali na haramu, kisha akasema: "Je unakubali kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye kubebwa?" Abul Hasan akajibu: "Kila chenye kubebwa ni chenye jufanyiwa kitendo, chenye kumtegemea kingine na chenye kubebwa ni jina pungufu katika tamshi , na mbebaji ni mtendaji(faa'il) na katika tamko kuna sifa, pia kama kauli ya mwenye kusema, juu na chini "Fawqa wa tahta, waa'alaa wa-asfali".

Mwenyezi Mungu mtukufu amesema: "Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri, basi ombeni kwayo." Hakusema, kwenye vitabu vyake kuwa yeye ni mwenye kubeba bali alisema yeye ni mwenye kubeba bara na baharini na mwenye kushika mbingu na ardhi, basi kinachobebwa ni asiyekuwa

Mwenyezi Mungu! Wala katu hajasikiwa yeyote aliyemuamini Mwenyezi Mungu na utukufu wake asema katika dua, 'Ewe uliyebebwa!."

Abu Qurrah Akasema: "Yeye amesema: "'Na wanaibebea Arshi ya Mola wako juu yao siku hiyo wanane…." Na akasema: "Wale wanaobeba Arshi?" Akasema Abul Hasan "Arshi sio Mungu na Arshi ni jina la elimu na uwezo na Arshi yake iko katika kila kitu, kisha akategemeza kubeba katika kitu kingine ambacho ni kiumbe miongoni mwa viumbe vyake kwani yeye alivilazimisha viumbe vyake kuibeba Arshi yake, na wao ni wabebaji wa elimu yake, na viumbe wanaogelea pembeni mwa Arshi yake na wao wanafanya kwa kutumia elimu yake na malaika wanaandika amali za ibada zake? Na akawalazimisha wanaoishi ardhini kutufu (kuizunguka) Nyumba Yake, na Mwenyezi Mugu "amelingana katika Arshi", kama alivyosema, Arshi na anayeibeba na aliye pembeni mwa Arshi Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwachukua, Mwenye kuwahifadhi, Mwenye kuisimamia kila nafsi, yuko juu ya kila kitu na haambiwi, "amebebwa au yuko chini."

Abu Qurra Akasema: "Je wewe unaikadhibisha riwaya hii iliyopokewa ikisema ati kwamba, Mwenyezi Mungu anapokasirika, basi hasira zake hujulikana kwa kuwa wale malaika wanaoibeba Arshi yake wanasikia uzito kwenye migongo yao, basi hupomoka kusujudu, na hasira ikiisha, basi Arshi huwa nyepesi na wakarudi kwenye visimamo vyao?

Abul Hasan akajibu: "Hebu niambie, tangu Mwenyezi Mungu alipomlani Ibilisi mpaka leo hii yeye amemkasirikia, basi ni lini hakuwa katika hali ya kukasirika? Naye kwa wasifu wako bado yuko vile vile amemkasirika Ibilisi, vipenzi vyake na wafuasi wake. Vipi unathubutu kumsifu Mola wako kuwa anabadilika kutoka hali moja hadi nyingine, na kwamba anapitiwa na yanayowapitia viumbe? Ametukuka! Mwenyezi Mungu hajabadilika na wenye kubadilika na uendeshaji uko chini yake na wote wanamuhitajia yeye naye ni Mkwasi, hamtegemei mwingine.

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 37



## Mas'ala 13

**Je mwawajua wa mwanzo zaidi waliopokea Hadithi za kumshabihisha Mwenyezi Mungu na kumfanya ana umbo?**

Wao ni: Umar bin Khattab, mwanawe Abdallah, Abu Musa Al-Asha'ari, mwanawe Abu Bakra, mtoto wa Amru bin Al-Asi na Abu Huraira na wote hao walikozipata ni kwa Kaabul akhbar!

Watawala wa Bani Umayya waliendeleza siasa ya Umar ya kuwaweka karibu mapadri na makasisi na wanafunzi wao na wakawaamrisha waislamu wajifunze kutoka kwenye elimu zao, mpaka marejeo yao yakajaa riwaya za wakristo hao na wakazinukuu kuzipeleka itikadi za Tawrat kwenye elimu za kiislamu, nao ni wengi kama vile: Muqatil bin Sulaiman Al-Balakhi, na wanafunzi wake, Wahbu bin Munabbih na ndugu zake, Abdallah bin Salaam na wanawe, Hasan Al-Basri na wanafunzi wake, Hamad bin Salma, na wengineo…

Kisha baadhi ya watawala wa ki-Abbas pia walifanya vivyo hivyo, hasa Al-Mutawakkil Al-Abbasi wakawafuata maimamu wenye itikadi ya umbo kama vile, Ahmad bin Hambal, Bukhari, AbuYaa'la Al-Muswili, Samnani, Darami, Abul Abbas Siraj, Is-haq Al-Handhwali na wengineo wenye kuamini kuwa Mola ana umbo na mwili, ambao waliieneza elimu ya mayahudi kwa waislamu.

Kwa hivyo tutatenga sehemu maalumu itakayozungumzia jinsi makhalifa wa kikuraishi walivyowafuata wanavyuoni wa kiyahudi na elimu zao.

## Maswali

**1.** Mnapofuta riwaya za Kaabul Akhbar na wanafunzi wake, na za Umar na mwanawe, na Abu Musa Al-Ash'aro na mwanawe, na mtoto wa Amr bin Al-Asi mtabaki na riwaya gani tena kwenu katika sifa za dini yenu,

ambazo waisilamu wanazizingatia kuwa ni kuamini umbo na tashbihi?

**2.** Mwasema nini juu ya aliyonukuu Dhahabi kutoka kwa Imam malik kwamba “Hadithi za kuwa na umbo” katika matabiina amezipokea mfanya kazi wa Bani Umayya na si mwanachuoni?

Amesema Dhahabi katika kitabu Siyaru a’alaamin nubalai Juz. 8 Uk. 103: “Abu Ahmad bin Adiyy: Ametuhadithia Ahmad bin Ali Al-Madaini, ametuhadithia Is-haq bin Ibrahim bin Jabir, ametuhadithia Abu Zaid bin Abil Ghamr, amesema Ibnul Qasim: “Nilimuuliza Malik juu ya Hadithi ambayo wamesema: “Kwamba Mwenyezi Mungu alimuumba Adam kwa sura yake, na hadithi iliyosema, kwamba Mwenyezi Mungu huufungua muundi (ugoko) wake, na kwamba huuingiza mkono wake kwenye Moto wa Jahannam na kumtoa amtakaye. Malik akakanusha hayo vikali sana, na akamkataza asiambiwe mtu yeyote. Akaambiwa, wenye elimu wanayazungumza hayo. Akauliza: “Ni nani huyo?” Akaambiwa: “Ibnu Ajlan kutoka kwa Abu Zanad. Akasema: “Ibn Ajlan hakuwa akiyajua haya na hakuwa mwanachuoni. Na Akatajwa Abu Zanad, akasema:”Huyu alikuwa ni mfanya kazi wao tu mpaka alipokufa.” (Malik aliposema ‘wao’ alikusudia Bani Umayya).

**3.** Lau zingelikuwa Hadithi hizi ni sahihi, nayo dhati na sifa za Mwenyezi Mungu ni miongoni mwa imani muhimu zaidi kiislamu, basi zingelikuwa zinajulikana sana na maswahaba wote wakati wa Mtume (s.a.w.w.), basi kwa nini maswahaba waliobaki hawakuzipokea bali walizikanusha?

## Mas’ala 14

### Wenye imani ya kuwa Mungu ana umbo huwakufurisha wenye kuwapinga, na huwatisha

Fatuwa yao imeenea ya kumkufurisha mama yao Aisha kwa sababu tu yeye

alisema kuwa ni uongo waliyoyapokea juu ya Mtume (s.a.w.w.) kuwa alimwona Mola wake, akasema: “Hilo ni kosa kubwa juu ya Mwenyezi Mungu mtukufu! Na mkali zaidi juu ya Aisha ni Ibnu Khuzayma, Sheikh wa Bukhari ambaye wanamwita Imamu wa maimamu, huyu amefikia hadi kumshambulia Aisha katika kitabu chake, ‘Tawhid.’

Amepokea Bukhari katika Sahih yake Juz. 6 Uk. 50: “Kutoka kwa Masruq, amesema, nilimwambia Aisha: “Ee mama, je Muhammad alimwona Mola wake?” Aisha akasema: “Nywele zangu zimesisimka kwa uliyoyasema. Uko wapi wewe na tatu alizokuhadithia, basi amesema uongo, aliyekuambia kuwa Muhammad alimwona Mola wake.” Kisha Aisha akasoma: “ Macho hayamfikii, naye huyafikia, naye ni Mpole, mwenye kujua. Haikuwa kwa mtu kuzungumza na Mola wake ila kwa wahyi, au nyuma ya pazia.” Na anayekwambia kuwa yeye anayajua ya kesho huyo amesema uongo. Kisha akasoma: “Na nafsi haijui nini itachuma kesho.” Na atakayekuambia kwa yeye ameficha, basi amesema uongo. Kisha akasoma: “Ewe Mtume, fikisha lile uliloteremshiwa kutoka kwa Mola wako.” Lakini yeye alimwona Jibril kwa sura yake mara mbili.”

Na katika Sahih Muslim Juz.1 Uk. 110: “ Kutoka kwa Aisha amesema: “Anayedai kwambaMuhammad alimwona Mola wake basi huyo amekuza ovu kwa Mola.”

Ibnu Khuzayma amemshambulia Aisha katika kitabu chake’Tawhid’ Uk. 225, akasema: “Hili neno nadhani Aisha alilisema wakati wa hasira, kungekuwa na neno zuri kuliko hilo ambalo tunaweza kujua anachokitaka ingekuwa ni vuzuri kwake. Si vizuri mtu aseme, Ibnu Abbas, Abu Dharri, Anas bin Malik, na kikundi cha watu, wote waseme ovu kubwa juu ya Mola wao, lakini mtu huzungumza kwa hasira neno ambalo linakuwa si zuri zaidi ya lingine.

Nasi twasema kama alivyosema Muammar bin Rashid alipotajiwa juu ya khitilafu ya Aisha na Ibn Abbas kwenye maudhui haya: Aisha kwetu si

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 40



mjuzi zaidi ya Ibnu Abbas na wanapohitilafiana ni muhali kusemwe kuwa Ibnu Abbas amesema jambo ovu kwa Mwenyezi Mungu, kwani yeye amethibitisha kitu ambacho Aisha amekikanusha.

Jambo hili lilikuwa na nguvu kwa wafuasi wa Hambali, Baghdad katika enzi ya Mutawakkil na baada yake, walikuwa na wafuasi waliokuwa wakiwashambulia watu wanaowapinga. Kumshambulia kwao Tabari kunajulikana, pale walipomuuliza juu ya kukaa juu ya Arshi kwa Mwenyezi Mungu, akakanusha dai la kuwa Mungu anakaa juu ya Arshi na ati Mtume (s.a.w.w.) anakaa kando yake. Wakataka kumuua, na alipofariki, walilivamia jeneza lake na wakazuia asizikwe kwenye makaburi ya waislamu!
Pia walimshambulia Ibn Habban msimulizi maarufu wa Hadithi kama walivyofanya kwa Tabari.

Amesema Al-Hamuwi katika kitabu ‘Mu’ujamul udaba’ Juz. 9 Uk. 18, 57 katika wasifu wa Tabari:”Tabari aliporejea Baghdad akitokea Tabarstan, baada ya kurejea kwake hapo, wakaanza kumpinga Abu Abdallah Al-Jassas na Jafar bin Arafa na Al-Bayadhi. Mahambali wakamwendea wakamuuliza juu ya Ahmad bin Hambali kuhusu msikiti wa Ijumaa siku ya Ijumaa na hadithi ya Mwenyezi Mungu kukaa juu ya Arshi. Abu Jafar akasema: “Ama Ahmad bin Hambal hitilafu yake haihesabiwi.” Wakasema: “Lakini wanavyuoni wamemtaja katika hitilafu za wanavyuoni.” Akasema: “Mimi sikumwona kuwa ilipokewa kutoka kwake wala sikumwona ana wenzake anaowategemea. Ama kuhusu Hadithi ya kukaa Mwenyezi Mungu juu ya Arshi, hiyo ni muhali.” Kisha akasoma shairi:
Ametukuka Mola asiye na mwenzi mliwazaji Wala hana anayekaa naye Arshini.

Mahambali waliposikia akisema hivyo, walimrukia na kumtupia vichupa vyao vya wino, na inasemekana walikuwa maelfu.

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 41



Akasimama Abu Jafar na kuingia nyumbani kwake wakaipiga mawe nyumba yake mpaka mlangoni kwake kukawa na kichuguu kikubwa!

Afande Nazuk akapeleka kikosi cha maelfu ya askari kikiwazuia watu na akasimama mlangoni kwake siku nzima hadi usiku na akamuru kuondolewa mawe hapo.

Na alikuwa ameandika shairi hilo alilolisoma hapo juu mlangoni kwake. Nazuk akaamrisha lifutwe.

Watu wa Hadithi badala yake mahali hapo wakapaandika shairi jingine:
Ahmadi ana cheo bila shaka ni cha juu pindi msafara utakapofika kwa Rahman. Atamsogeza na kumkalisha akiwa mkirimiwa japokuwa katika heshima yupo hasidi.

Juu ya Arshi akiwa amemfunika kwa manukato akiwa juu kuliko mjeuri na mpingaji.

Ni kweli anastahiki heshima hii ya pekee, kama ile aliyoipokea Laythu kutoka kwa Mujahidu**.**"

Kisha akatoka nyumbani kwake na akaandika kitabu chake mashuhuri cha kuomba msamaha na akataja madhehebu yake na itikadi yake, akamponda anayedhani kinyume na hivyo, akakisoma kwa watu na Ahmad bin Hambal huku akimfadhilisha, akataja madhehebu yake na usahihi wa itikadi yake. Na hakuacha kumtaja mpaka alipofariki, na hakutoa kitabu chake cha hitilafu za wanavyuoni mpaka alipokufa, wakakikuta kimezikwa mchangani, wakakitoa na kutoa nakala, hivi ndivyo nilivyosikia kutoka kwa jamaa miongoni mwao ni baba yangu."

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 42



## Maswali

**1.** Nini maoni yenu juu ya atikadi ya mama yenu Aisha aliyehukumu kwamba anayedai kuwa Mtume (s.a.w.w.) alimwona Mola wake basi amefanya kosa kwa Mwenyezi Mungu? Je Ibnu Taymiyya na wafuasi wake wamefanya kosa kubwa kwa Mola wao? Je hii ina maana ni kuwakufurisha? Na je Aisha kwa hukumu yake hii ni mwenye kumpwekesha Mungu, ni mshirikina au amepotea?

**2.** Hatujaona Hadith katika marejeo ya Sunni kuhusu kuona katika Israi ila ya swali la Abu Dharri na swali la Aisha kwa Mtume (s.a.w.w.) na ilikanushwa katika mbili hizo kuonekana Mungu kwa macho, na wale wanaonasibisha kwa Mtume kumwona hawajapokea Hadithi kwake hata moja kwamba yeye alimwona Mola wake kwa macho yake, bali walisema hivyo kwa ijtihad yao tu. Hivyo ukweli hakuna mkabala ila ni ijtihadi na si Hadithi, kwani kwa mujibu wa hadithi ya Abu Dhari na Aisha ni kuwa Mtukufu Mtume alikanusha kuonekana kwa macho.

Ama riwaya ya Ibn Abbas ni yenye kupingana, hivyo hapana budi waiporomoshe na kurejea kwenye asili ambayo ni kukosa kuthibitisha hilo ila kwa dalili.

Ibnu Khuzayma mwenyewe kabla ya kumshambulia Aisha amenukuu Hadithi kutoka kwa Ibn Abbas inayopinga kuona kwa macho.Je mwasemaje?

**3.** Nini maoni yenu juu ya aliyoyasema Sheikh Muhammad Abduh katika Tafsir Al-Manar, Juz. 9 Uk. 148: “Tambua kuwa yaliyotangulia ni kwamba uthibitisho uliyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas ndio unaosihi kusemewa yale yaliyodaiwa kuwa ni makosa pindi Aisha alipokanusha, kwani wenyewe ni ijtihadi kutoka kwake mwenyewe. Hakuna Hadithi *‘marfuu’* kwake na kwamba kilichoswihi kwake kuhusu kuona kwa moyo kinapinga ile iliyoswihi katika tafsiri ya Mtume ya Aya mbili za

Surat Najmi, nayo ni kuwa Aya mbili hizo zinahusu kumwona (s.a.w.w.) Jibril kwa sura yake aliyoumbiwa na Mwenyezi Mungu.

Zaidi ya hapo ni kwamba haiko mbali kuwa riwaya ya Ikrima ni miongoni mwa alizozisikia kutoka kwa Kaabul Akhbar ambaye Muawiya (Mpokezi) amesema juu yake kuwa, tulikuwa tukimwona kuwa ni mwongo, kama ilivyo katika Sahih Bukhari.

Na riwaya ya Ibnu Is-haq haizingatiwi katika daraja hii kwani ina udanganyifu, naye ni mwenye kuaminiwa katika vita si katika Hadithi.

Na akasema katika tafsir Al-Manar Ju. 9 Uk. 139: “Na Aisha naye ni katika mafasaha wa kikuraishi anakanusha kuonekana kwa macho kwa kutumia tamko “macho hayamfikii” kama dalili huku akijua tofauti ya kimaana iliyopo kati ya maana hizo mbili. Na anatoa dalili pia kwa kauli yake Mwenyezi Mungu: “Na haikuwa kwa mtu aseme na Mwenyezi Mungu ila kwa wahyi au nyuma ya pazia.” Wamechukua hii na ile katika kuthibitisha kutokuonekana Mungu katika maisha haya ya duniani, lakini ni muhali Mungu kuonekana kwa macho Akhera, kama vile duniani.

**4.** Je mnaafikiana na vitisho hivi vya kimawazo walivyovifanya baba zenu kuwafanyia Tabari na Ibnu Habban na wengineo, na wanavyofanya baba zenu na watoto wenu kwa waislamu hasa katika haram mbili tukufu?

**5.** Nini maoni yenu juu ya Tabari na Ibnu Habban, je wao ni waislamu kwenu au ni makafiri?

## Mas’ala 15

### Msimamo wenu juu ya Hashawiyya ni upi?

Baadhi ya watafiti wanaonelea kuwa hawa mahashawiyya ni mahambali wenye imani ya Mungu kuwa na umbo, na wana visa vingi juu ya hilo, na

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 44



katika kukusanya Hadithi za Israiliyya na kuzieneza, imefikia madai yao kuwa hata baadhi yao walimwona Mungu duniani, kwamba yeye ni kijana mwenye nywele zilizosokotana au walimwona akipanda ngamia au punda!

Abu Zahra amesema katika kitabu 'A-madhahibul Islamiyya Juz. 1 Uk. 232: "Ibnul Jawzi amesema katika hilo: "Nimeona katika watu wetu wanaosema katika misingi ya dini yasiyofaa..wakatunga kitabu kilichoyachafua madhehebu nimewaona wameshuka daraja hadi la wasiojua, wakazichukua sifa kulingana na milango ya fahamu wakasikia kuwa Mwenyezi Mungu amemuumba Adam kwa sura yake basi wakamthibitishia sura na uso kuzidi dhati yake na mdomo na meno, mng'aro wa uso wake, mikono miwili na vidole viwili, kiganja kidole gumba, kidole kidogo, kifua, paja mindi miwili, miguu miwili, na wakasema, tumesikia pia kutajwa kichwa! Wamechukua maana ya dhahiri katika sifa za majina ya Mwenyezi Mungu wakaziita kwa sifa za majina ya kuzushwa na hawana dalili yoyote juu ya hilo ya kupokea wala ya kiakili, na hawakutafiti nasi zinazosarifu dhahiri ya maana na kupeleka kwenye maana zinazompasa Mwenyezi Mungu, wala zinazotokomeza sifa za kuzuka zitokanazo na dhahiri za maneno.

Na hawakutosheka na kusema tu sifa ya kitendo bali hata sifa ya dhati, kisha walipothibitisha sifa hizo wakasema, hatuzichukulii kilugha, mfano, mkono kwa maana ya neema na uwezo, na kuja, kwa maana ya wema na upole, bali wamesema kuwa wanachukulia mtazamo wa kijamii, na mtazamo wa kijamii ni sifa za wanaadamu, na kitu huchukuliwa kwa maana yake halisi ikiwezekana, na akisarifu mwenye kusarifu huichukulia kwa maana ya kinaya, kisha wanahangaika kuhusu tashbihi na wanakimbia isinasibishwe kwao, hivyo wanasema: "Sisi ni Ahlu Sunna! Na maneno yao juu ya tashbihi yako wazi.

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 45



## Maswali

**1.** Maoni yenu ni nini juu ya aliyoyasema Ibnul Jawzi ambaye yeye ni katika maimamu wa mahambali?

**2.** Nini maoni yenu juu ya Ibnu Asakir alivyosema juu ya mababu zenu wa kihasahawiyya, ambapo katika kitabu chake, Tabyiinu kidhbil muftara Juz. 1 Uk. 310 amesema: "Hakika watu wa kihashawiyya wanaojiita mahambali wameonyesha bidaa mbaya hapo Baghdad ambayo hata mlahidi haisamehe, wachilia mbali mwenye kumpwekesha Mwenyezi Mingu. Wala haimfai pia mwenye kupinga asili ya sharia wala mwenye kutomlinganisha Mungu na sifa yoyote; na wamenasibisha kila linalomtakasa Mwenyezi Mungu dhidi ya mapungufu na maafa; na wanakanusha kwake uzukaji na mfanano, na wanamtukuza dhidi ya kugeuka na kutoweka na wanamtukuza dhidi ya kubadiika kutoka hali moja hadi nyingine na kugeuka katika matukio na kuzuka matukio kwake, mpaka kwenye ukafiri na upotevu na kuwapinga watu wa haki na imani!

Wamewaponda maimamu waliotangulia na kuleta kasumba katika dini, na wakawalaani katika misikiti ya ijumaa na katika mabaraza, misikitini na kwenye hafla, hata masokoni, barabarani, faraghani na kwenye jamaa, kisha tamaa ikawaghuri na kuwapeleka kwenye upotofu wao katika kuwatukana wale wanaotegemawa kuwa ni maimamu wa uongofu na ni kamba imara katika sharia, wakavifanya vitendo vya kidini kuwa ni maasi dhalili, wakazidi hata kumvunjia heshima Shafii (r.a.) na wenzake. Ikawafiki kurudi kwa Sheikh Imam Abi Nasri bin Ustadh Imam Zainul islam, Abul Qasam Al-Qashiri hapo Makka na akawaita watu kwenye Tawhid na kumtukuza Mwenyezi Mungu dhidi ya matukio na kuwekewa mipaka, watu wa uhakiki wakamkubalia miongoni mwa watu bora na mabwana wakubwa.

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 46



Hashawiyya wakazidi kwenye upotofu wao na kung'ang'ania ujinga wao na wakakataa ila kusema kuwa Mwenyezi Mungu ana miguu, meno, taya, na vidole na mwenyewe hushuka na kupanda punda akiwa na sura ya kijana mzuri mwenye nywele za paka, akiwa amevaa taji linalong'ara miguuni akiwa na sandali za dhahabu! Hilo wakalihifadhi na kulieneza wakaliandika katika vitabu vyao na kuwaambia watu Hadithi hizi hazina taawil, bali zinachukuliwa kidhahiri tu, na zinaaminiwa kama zilivyotajwa maneno yake, na kwamba Mwenyezi Mungu anazungumza kwa sauti kama ya radi, kama mlio wa farasi!

Na wanawatesa watu wa haki wanaosema kuwa Mwenyezi Mungu anasifika kwa sifa za utukufu, anasifika kwa elimu, uwezo, usikizi, uoni, uhai, utashi na kusema, na hizi ni sifa za kale na kwamba Yeye mtukufu ameepukana na kubadilika na haifai kuifananisha dhati yake na ya viumbe, wala maneno yake yawe kama maneno ya viumbe,
Na iliyo mashuhuri ni kwamba maimamu mafakihi bila kujali tofauti za madhehebu zao katika mamabo ya matawi ya dini, walikuwa wakiieleza wazi wazi itikadi hii na wakiisomesha wazi wazi kwa watu wao na anayekwenda kuishi kwenye miji yao na wala hakuthubutu hata mmoja wao kuikanusha wala kuwapinga, hii ndio itikadi ya watu wa Shafii wanamfuata Mwenyezi Mungu mtukufu." Je ni yapi maoni yenu?

**3.** Ni nini msimamo wenu juu ya mahashawiyya wale wa mwanzo kujiita 'Ahlu-Sunna', je mnaona kwamba wao ni masalafi wenu katika masunni?

**4.** Ikiwa itikadi yenu kwa sifa za hisi kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ni ijtihadi kutoka kwenu, kwa nini basi mnazuia ijtihad ya wengine? Na kumhukumu kuwa kafiri na mpotevu yule anayemtakasa Mwenyezi Mungu mtukufu dhidi ya sifa za kuhisi?

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 47



## Mas’ala 16

### Wanaharamisha taawil, na wao wanaifanya, wanakataa kinaya, na wao wanaitumia

Madhehebu ya Ibn Taymiyya yamesimamaia msingi wa Mungu kuwa na umbo kwa msingi batili wa kuwa ni haramu kutaawili sifa za Mwenyezi Mungu na inapasa kuzichukulia sifa hizo kwa dhahiri kimaada! Akasema: “Hakika mkono wa Mwenyezi Mungu katika kauli yake: “Hakika wale wanaokubai, hakika si jingine, wanambai Mwenyezi Mungu, mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao basi anayetengua basi anaitengua kwa ajili ya nafsi yake, na anayetekeleza kile alichomuahidi Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu atampa malipo makubwa.”

Maana yake-ati-Mwenyezi Mungu ana mkono nao ni wenye kujeruhi kama mikono yetu.” Na waislamu wakampinga kwa hilo waliosema kuwa maana ya neno ‘Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao’ hiyo ni kudra yake ambayo iko juu ya uwezo wao. Ametukuka Mweyezi Mungu dhidi ya kuwa mwenye kuhisika na dhidi ya kuwa na viungo vyenye kuhisika kama vyetu.

Lakini utawaona wanaitumia taawili ambayo wao wameikataza, wanapobanwa na hoja, na hasa wanapofikia kwenye fadhila za Ahlul-bait amabao hawawapendi au inapokuwa katika kuwalaumu Bani Umayya ambao wao wanawapenda!

Kwa sababu ya msingi huu batili wamelazimika kukanusha uwepo wa kinaya katika Qur’an na Sunna kwa kudai kuwa, kila maneno ni lazima yachukuliwe kwa maana yake ya kilugha ya kimaada, wala haifai kuchukuliwa kwa maana ya kinaya au kufanyiwa taawili.

Wakati Qur’an au Hadithi inaposema, ‘Mkono wa Mungu, au jicho la Mungu, au uso wa Mungu, ‘ maana yake ni kuwa Mungu ana mkono, na

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 48



jicho, na uso kikweli si kikinaya na anaposema, “kila kitu kitaangamia ila uso wake,” maana yake kwao ni kuwa Mungu atatoweka na utabaki uso wake tu!
Lakini anaposema Mtume (s.a.w.w.) “Je mimi si bora kwa waumini kuliko nafsi zao? Wakasema: “Kwa nini wewe u mbora.” Akasema: “Basi atakayekuwa mimi ni bwana wake na Ali pia ni bwana wake.” Hapo utawaona wanachukua taawili ili waepuke makusudio yake.

Sheikh wao Ibn bazi amesema katika Fatawa Juz. 4 Uk. 382: “Iliyo sahihi kwa wahakiki (ni kina nani hao?) ni kwamba katika Qur’an hakuna ile kinaya wanayoifahamu watu wa fani ya ufasaha wa lugha, bali kila kilichomo humo ni uhakika ulioko mahali pake.’

## Maswali

**1.** Qur’an imeshuka kwa lugha ya kiarabu, nayo imejengwa kwa uhakika, kinaya, fumbo, tashbihi, istia’ara na mengineyo katika mbinu za elimu ya ufasaha wa lugha.

Maamun alimuuliza Imam Ridha (a.s.) kuhusu kauli yake Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake:

﴿ عَفَا ٱللَّهُ عَنكَ لِمَ أَذِنتَ لَهُمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ وَتَعْلَمَ
ٱلْكَٰذِبِينَ ﴿٤٣﴾ ﴾

**“Mwenyezi Mungu amekusamehe, kwa nini umewaruhusu mpaka ibainike kwako wale waliosema ukweli na uwajue waongo.” (Tawba: 43.**

Akasema (a.s.): “Hii ni miongoni mwa zile zilizoteremka kwa mtindo wa, nakwambia wewe nataka asikie jirani. Mwenyezi Mungu alimwambia hivyo Mtume wake na akikusudia umma wake. Na pia kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu: “Hakika ulipewa wahyi na kwa wale waliokuwa kabla yako, kama ukimshirikisha (Mwenyezi Mungu) bila

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 49



shaka amali zako zitaruka patupu, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kupata hasara (Zumar: 65) (Kitabu: U'yuunul akhbari ridhaa Juz. 2 Uk. 180) je ni ipi dalili yenu ya kukataa kinaya katika Qura'n?

2. Kwa kauli yenu ya kukataa kinaya katika Qur'an na Sunna inawalazimu matokeo mengi ya ubatilifu ambayo hamuwezi kuyatekeleza, mnafasiri vipi kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.):

﴿ وَلَا تَدْعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ ۘ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ كُلُّ شَىْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُۥ ۚ لَهُ ٱلْحُكْمُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٨﴾ ﴾

**"Wala usimuombe pamoja na Mwenyezi Mungu, mungu mwingine, hapana Mola isipokuwa Yeye, kila kitu ni chenye kuangamia ila Yeye. Hukumu iko kwake na kwake mtarejeshwa." (Al-Qasas: 88).**

Je, mnasema -Mungu apishie mbali- kwamba Mwenyezi Mungu ataangamia ila uso wake?

3. Ikiwa mnaamini uharamu wa taawili na hivyo mnaharamisha taawili ya Aya zenye maana iliyofichikana kwa nini basi mnapingana nyinyi wenyewe mnajichanganya katika taawili za Aya zilizo wazi ambazo zinakanusha tashbihi na kule kumpa Mungu umbo, na hamchukui ilivyo dhahiri na mnazitafsiri Aya zenye maana iliyofichikana kupitia Aya zilizo wazi, kama wafanyavyo waislamu wengine?

Miongoni mwa Aya zilizo wazi ni ile isemayo: "Huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu, hapana mola anayeabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, Muumba wa kila kitu, basi muabuduni yeye (tu), naye ni Mlinzi wa kila kitu. Macho hayamfikii (hayamuoni) bali Yeye huyakifikia macho (kwa kuwaonea hao wenye macho), naye ni Mwenye kujua yaliyofichika na yaliyo dhahiri." (An'aam: 102-103).

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 50



Nyingine: “Yeye ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi amekuumbieni wake (zenu) kutoka kwenye jinsi zenu, na wanyama nao akawaumbia wake zao (katika jinsi moja na wao), anakuzidishieni kwa namna hii. Hakuna chochote mfano wake, naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona. (Shuraa: 11).

Nyingine:

﴿ وَٱضْمُمْ يَدَكَ إِلَىٰ جَنَاحِكَ تَخْرُجْ بَيْضَآءَ مِنْ غَيْرِ سُوٓءٍ ءَايَةً أُخْرَىٰ ﴿٢٢﴾ ﴾

**“Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala wao hawawezi kumjua (Mungu) vilivyo. (Twaha:110).**

Nyingine:

﴿ ٱلَّذِى جَعَلَ لَكُمُ ٱلْأَرْضَ فِرَٰشًا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءً وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَخْرَجَ بِهِۦ
مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا۟ لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾ ﴾

**“Ambaye amekufanyieni hii ardhi tandiko na mbingu kuwa kama paa.Na akawateremshia maji kutoka mawinguni; na kwa hayo akawatolea matunda yawe riziki zenu, basi msimfanyizie Mwenyezi Mungu washirika, na hali mnajua.” (Baqara: 22)**

Nyingine ni: “Alipofika Musa katika miadi yetu na Mola wake akazungumza naye, akasema:”Eee Mola, nionyeshe nikuone,” Mola akasema: “Hutaniona, lakini angalia jabali, likitulia mahali pake huenda ukaniona. Basi Mwenyezi Mungu alipojionyesha (kuonyesha baadhi ya ishara zake) kwenye jabali akalifanyia lipasuke, akaanguka Musa amezimia, na alipozinduka alisema:

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 51



﴿ فَلَمَّآ أَفَاقَ قَالَ سُبۡحَٰنَكَ تُبۡتُ إِلَيۡكَ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ١٤٣ ﴾

**“Utakasifu ni wako nimetubu kwako nami ni mwanzo wa wenye kuamini.” (A’araaf: 143).**

Nyingine ni : Na mliposema: “Ee Musa, hatutakuamini mpaka tumuone Mungu wazi wazi.” Yakawanyakueni mauti ya ghafla (ya moto wa radi) na hali mnaona. (Baqara: 55).

Nyingine: “Wanakuuliza watu wa kitabu uwateremshie kitabu kutoka mbinguni, na kwa hakika walimuuliza Musa makubwa zaidi ya hayo, wakasema: “Tuonyeshe Mungu wazi wazi.” Ukawachukua moto wa radi kwa sababu ya upotevu wao. Kisha wakamfanya ndama kuwa mungu baada ya kuwajia wao hoja za wazi, lakini tukalisamehe hilo na tukampa Musa hoja zilizo dhahiri juu yao.” (Nisaa: 153).

Nyingine: “Wakasema wale wasiotarajia kukutana nasi, ‘Lau kama tungeliteremshiwa malaika au tumuone Mola wetu, hakika wamefanya kiburi ndani ya nafsi zao na wamepetuka mipaka kabisa.”

Nyingine: “Sema, Yeye Mwenyezi Mungu ni mmoja, Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kutegemewa, hakuzaa wala hakuzaliwa, wala hakuna na anayefanana naye.” (Ikhlas).

Kwa nini basi mwasema taawili ni haramu? Kisha mnafanyia taawili zote kwa tashbihi?

**4.** Ikiwa Qur’an yote ni maneno ya ‘hakika’ tu na taawil ni haramu, basi na Hadithi zote ni hakika tu na taawil pia ni haramu, mna nini hamwachi Hadithi yoyote ya Mtume (s.a.w.w.) inayopinga maoni yenu isipokuwa hapo ni lazima mtaifanyia taawil?

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 52



5. Maadamu taawil kwenu ni haramu, basi na kinachotoka kwenye taawil pia ni haramu na ni kosa. Vipi sasa katika tafsiri yenu ya Qur'an au Hadithi mnategemea taawil yenu au ya wenye kuawili, na mnajenga madhehebu yenu kwenye haramu na uovu?

6. Maadamu taawil kwenu nyinyi ni haramu, basi hapana tofauti ifanywe na nyinyi au ifanywe na mwingine, vipi nyinyi mnatafuta aliyeitolea taawili Aya au Hadithi kisha mnamtegemea? Nyinyi mfano wenu ni kama aliyetoa fatuwa ya kuharamisha nyama ya kafara kisha akatafuta anayeihalalisha ili apate kuila? Je mmemsikia Talmanki mtoaji taawili aliyekutwa na imam wenu Ibnu Taymiyya na imam wenu Ibn Baaz?

Amesema Ibn Baaz katika fatawa yake Juz. 1 Uk. 148: "Amesema Abu Umar Talmanki (Mungu amrehemu): Waislamu wa Ahli sunna wamekongamana kwamba maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t.): "Naye yu pamoja nanyi." Na mfano wa hiyo katika Qur'an, kwamba hiyo ni elimu yake, na kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu yuko juu ya mbingu kwa dhati yake ametulia juu ya Arshi Yake, kama kilivyosema kitabu chake."

Ibn Baaz, ni kama imam wake, ametegemea juu ya taawil ya Talmanki na kongamano la waislamu ambalo kalidai huyo Talmanki
Ikiwa litasihi kongamano lao basi itakuwa ni kongamano la taawili inayopinga kuiharamisha kwenu, na kama haikusihi, basi haina manufaa yoyote kwenu taawil ya Talmanki. Nini maoni yenu?

## Mas'ala 17

**Nini maoni yenu juu ya Hadithi hizi zilizowekwa?**

Ama sisi na waislamu wote wanaomtakasa Mwenyezi Mungu tunaitakidi kuwa ni Hadithi zilizowekwa (*marfuu'*) ili kuyapa nguvu madhehebu ya Kaabul Akhbar na watu kama yeye wenye kufanya tashbihi na kumpa

Allah umbo, ikisihi Hadithi mfano wa hizo basi hapana budi kuwa na taaw-il yake, kwa sababu kanuni ya lugha ya kiarabu inasema kuwa, neno huchukuliwa kwa maana yake ya hakika, mpaka kutokee kizuizi cha kimatamshi au cha kiakili, ndipo huchukuliwa maana ya kinaya.

- Wao wamesema: "Mwenyezi Mungu Mtukufu anasikia na kuona kama asikiavyo na aonavyo mwanaadamu!"
- Wamesema: "Mtume alimwona Mola wake akiwa Mola ni kijana, mwenye nywele zilizosokotana, amesimama kwenye ardhi ya manyasi ya kijani kibichi, akiwa amevaa sandali mbili za dhahabu."
- Wamesema: "Yeye ana macho miwili mazima, ama Dajjal ni chongo.
- Wamesema: "Ana mikono miwili, macho, miguu na viungo."
- Wamesema: "Anaweza kuwa na sikio au anaweza kuwa hana sikio lakini ana ubavu na kiuno."
- Wamesema: "Yeye (Allah) anatembea kwa miguu, huenda akakimbia na kukazana."
- Wamesema: "Kwamba Yeye Mola (s.w.t.) anaiona dunia kwa macho."
- Wamesema: "Anavaa juba na hupanda ngamia."
- Wamesema: "Ni kijana mzuri, mwenye nywele zilizosokotana, na huvaa sandali mbili za dhahabu."
- Wamesema: "Anakasirika kama akasirikavyo mwanaadamu, na kwamba anacheka duniani na akhera."
- Wamesema: "Atadhihiri kwa waja wake akiwa yu katika hali ya kucheka."

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 54



- Wamesema: “Alimchekea Talha na Saad.”
- Wamesema: “Hucheka na huendelea kucheka.”
- Wamesema: “Kusema kwake sauti yake ni kama radi, na kucheka kwake ni kama umeme.”
- Wamesema: “Atadhihiri kwa umbo, hasusan kwa Abu Bakr.”
- Wamesema: “Anakaa juu ya Arshi na Arshi yake ina mlio, mbinja na sauti kwa uzito wake.”
- Wamesema: “Yeye ni mzito kuliko chuma.”
- Wamesema: “Jua kila siku hushuka chini ya Arshi.”
- Wamesema: “Wabebaji wa Arshi ni wanyama, kama ilivyotajwa katika Tawrat.”
- Wamesema: “Wabebaji Arshi ni malaika wakisufi, wanaozungumza kiajemi.
- Wamesema: “Anakaa kitini wake na kughibu dhidi ya dunia na pembeni mwake wako manabii wakiwa wamekaa vitini.”
- Wamesema: “Atakaa Abu Bakr juu ya kiti mbele ya Arshi.”
- Wamesema: “Atakaa rafiki waAhmad bin Hambali juu ya zulia la Arshi.”
- Wamesema: “Pepo ya Aden ndiyo maskani ya Mwenyezi Mungu, na Arshi yake iko hapo.”

- Wamesema: “Anaona kwa macho akhera na kuona kwake kwa macho ni katika ladha kubwa kabisa.”

- Wamesema: “Anaonyesha muundi, au miundi yake na kuwasamehe wanafiki.”

- Wamesema: “Anakaa juu ya daraja na kuweka mguu wake juu ya mwingine.”

- Wamesema: “Moto haujai mpaka Mungu aweke mguu wake humo.”

- Wamesema: “Mwenyezi Mungu mtukufu ana mwili ambao hushuka duniani kila usiku.”

- Wamesema: “Mwenyezi Mungu hushuka usiku wa nusu ya mwezi wa Shaaban, pia siku ya Arafa.”

Mpaka mwisho wa kauli zao na uzushi wao….!!!

## Maswali

**1**. Je hamwoni kuwa Hadithi za tashbih na kumpa Mungu umbo, zimepokewa na walioathirika na mawazo ya kiyahudi? Ambao Mtume (s.a.w.w.) aliwaita ‘Al-mat-hukun na akawatahadharisha waislamu na watu hao?

**2.** Ni nassi zipi mnazozikubali katika hizi na ni zipi mnazozikataa?

**3.** akati Mwenyezi Mungu anaposhuka ardhini, kama mnavyodai, je hupanda au hapandi?

**4**. Mnadai kuwa Mola wenu hushuka kila usiku, na daima dunia yote siku zote ina usiku, sasa hushuka kwa kufuata saa za eneo lipi?

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:28 AM Page 56



## Mas'ala 18

**Kauli yao kuwa kuna uwili baina ya dhati ya Mwenyezi Mungu na sifa zake**

Sifa za Mwenyezi Mungu za dhati kwetu sisi ndio dhati yake yenyewe Aliye Mtukufu, hakuna uwili kati ya mbili hizo, ambapo wenye kupinga wanasema kuwa, sifa dhati si dhati yake, inalazimu katika kauli yao iwe dhati ya kimungu tukufu ni yenye kuundika na sehemu mbili, kwa sababu sifa ni kitu kingine na dhati ni kitu kingine!

Aswaduq amesema katika kitabu chake At-Tawhid Uk. 243: "Kutoka kwa Hisham bin Al-Hakam kutoka katika Hadithi ya Zandiq na Imam Jafar Sadiq (a.s.) ikawa miongoni mwa kauli za Imam Jafar Sadiq kwake ni: "Kisha ukidai kuna mbili hapana budi itakupasa kuwe na uwazi (nafasi) kati yao wa tangu milele, na nafasi itakuwa ni ya tatu kati yao, ukidai tatu, itakulazimu ile hali tuliyoisema kwenye mbili, mpaka kati yake kuwe na mipenyo miwili hivyo itakuwa tano, kisha itaongezeka idadi mpaka kufikia isiyo na mwisho kwa wingi.

Na amesema katika Uk. 83: "Bedui mmoja alisimama siku ya vita ya Jamal kwa Amirul muuminina (a.s.) akasema: " Ee kiongozi wa waumini, unasema kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja?" Wakasema: "Ee bedui, je humuoni huyu ewe Amirul muuminina ana kugawanya moyo?" Akasema Anmirul muuminina: "Mwacheni, kwa sababu kile anachokitaka ndicho tunachokikusudia kwa watu." Kisha akasema: "Ee bedui, kauli ya kusema kwamba Mungu ni mmoja imegawanyika vifungu vinne: Sehemu mbili za kwanza hazijuzu kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, na sehemu mbili zinathibiti kwake. Ama zile ambazo hazijuzu kwake ni kauli ya mwenye kusema, mmoja, akikusudia mlango wa kuhesabu, hii haijuzu, kwa sababu kisicho na cha pili hakiingii katika mlango wa kuhesabu, je huoni alikufuru mwenye kusema, nafsi moja ndani ya tatu."

Na kauli ya mwenye kusema, yeye ni mmoja katika watu, akikusudia aina ya jinsi; hii haijuzu kwa sababu hii ni tashbihi na Mola wetu ametakasika na hilo.

Ama aina mbili zinazothibiti kwake ni: Kauli ya msemaji, Yeye Mungu ni mmoja hakuna katika vitu anachofanana nacho, hivyo ndivyo alivyo Mola wetu.

Na kauli ya mwenye kusema, Yeye mtukufu ni mpweke wa kimaana, yaani Yeye hagawanyiki katika kuwapo kwake, katika akili na katika mawazo, hivyo ndivyo alivyo Mola wetu."

Katika maneno yao kumepatikana uwili, wao wamesema kuwa Qur'an ni maneno ya Mwenyezi Mungu nayo ni sehemu ya dhati yake, naye ni wa kale, hakuumbwa!

Maimamu wa Ahlul bait wamewajibu kuwa Qur'an ni maneno ya Mwenyezi Mungu nayo yameumbwa, sio maana ya kuwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu ni kuwa hayo ni sehemu ya dhati Yake bali maana yake ni kuwa Mwenyezi Mungu ameiumba , akairidhia na akainasibisha na nafsi yake. Amesema (s.w.t.): "Hayawajii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao ila huyasikia, na hali wanafanya mchezo." (Anbiya: 2).

## Maswali

**1.** Maadamu sifa za Mwenyezi Mungu mtukufu si dhati yake kwenu nyinyi, je ni kipi kilikuwa kabla ya kingine?

**2.** Ikiwa sifa za Mwenyezi Mungu si dhati yake, basi inalazimu awe Mungu ni mwenye vifungu vilivyoungana. Je mnakubali hilo?

**3.** Vipi mnaifasiri kauli yake Mwenyezi Mungu: "Hayawajii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao ila huyasikia, na hali wanafanya mchezo."

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:29 AM Page 58



## Mas'ala 19

**Nini msimamo wenu juu ya wanavyuoni wa madhehebu manne na wafuasi wao?**

Msimamo waliosimama maimamu wa madhehebu wa kale, kisha katika zama zetu hizi, ni dhidi ya kusema kwamba Mungu ana tashbihi na umbo, kama wasemavyo mahambali na Ibn Taymiyya aliyeuhisha msimamo huu. Wanavyuoni wametunga vitabu vingi katika kumtakasa Mwenyezi Mungu na kukataa kumshabihisha, na miongoni mwa watunzi maarufu, ambao si Shia, ni: Al-Bayhqi, Sabki Shafii, Ibnul Jawzi Hambali, Fakhru Razi Ash'ari, Mahdi Ibn Tarmut Maliki, na wengineo.

## Maswali

**1.** Je mnawahukumu kwa ukafiri maimamu wa madhehebu manne na wafuasi na opotevu kwa sababu wengi wao ni Asha'ri na baadhi yao ni Mu'utazila?

**2.** Je mnawahukumu kwa ukafiri wanavyuoni wa Asha'ira kwa sababu wao wamezisimamisha hoja zenu?

**3.** Nini maoni yenu juu ya Hadithi nyingi zinazobatilisha madhehebu yenu katika tashbihi na ambayo ameipokea Al-Bayhaqi katika kitabu chake, Al-asmau was sifaat na vingine, je mwajibu au mwafanya taawili?

## Mas'ala 20

**Kuwatupia Shia itikadi yenu ya tashbihi na kumpa Mungu umbo**

Katika kitabu, 'Usul madh-habi shial imamiyyah' cha Nasir Al-Faqari Juz. Uk. 527 amesema: "Sehemu ya tatu: Itikadi yao juu ya majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake. Mashia katika sehemu hii wana mapotevu

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:29 AM Page 59



manne:
La kwanza: Upotevu wa kupetuka mipaka katika kuthibitisha, uitwao kumpa Mungu umbo.

La pili: Kuondoa ukweli wa Aliyetukuka Mola mtukufu kutokana na majina na sifa zake.

La tatu: Kuwasifu maimamu kwa majina ya Mwenyezi Mungu na sifa zake.

La nne: Kuzipotosha Aya kwa ajili ya kulinda imani ya kutolinganisha majina na sifa.

Nitasimama kueleza kila suala miongoni mwa masuala haya manne, na nitabainisha madhehebu ya Shia ndani yake:

Utafiti wa kwanza: Upotevu wa kupetuka mpaka katika kuthibitisha (kuwa na umbo).

Huu ulienea baina ya mayahudi lakini wa kwanza aliyezusha hilo kwa waislamu ni marafidhi ndipo juu ya hili emesema Razi: "Mayahudi wengi wao ni wenye kushabihisha na kushabihisha mwanzo kulianzwa na marawafidhi kama vile Hisham bin Al-Hakam, Hisham bin Salim Al-Juwailiqi, Yunus bin Abdurahman Al-Qummi na Abi Jafar Al-Ahwal.

Na walikuwa hao waliotajwa ni wale ambao mashia wanawaheshimu kama mashekhe wao na ni waaminifu katika kunukuu madhehebu yao.

Sheikh Ibnu Taymiyya amempanga wa kwanza aliyesema neno hili baya katika hao, akasema: "Mtu wa kwanza aliyejulikana katika Uislamu kusema kuwa Mwenyezi Mungu ana umbo ni Hisham bin Al-Hakam."

Na kabla ya hapo Ametaja Ash'ari katika kitabu maqaalatul islamiyya

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:29 AM Page 60



kwamba mashia wa mwanzo mwanzo walikuwa wakisema kuwa Mwenyezi Mungu ana umbo, kisha akabainisha madhehebu yao katika jambo hili, na hata akanukuu baadhi ya maneno yao katika suala hilo ila yeye anasema kuwa kuwa waliokuja mwisho baadhi wameenda kinyume na wakaelekea kwenye kutofananisha. Na hii inajulisha kuwa mwelekeo wa Shia katika kutofananisha ulikuwa ni wa hivi karibuni, tena yatakuja maelezo yaliyosemwa katika ukomo huo.

Watu wa vikundi wamenukuu maneno yanayonasibishwa na Hisham bin Al-Hakam na wafuasi wake ambayo yanafanya ngozi za wenye kuyasikia zisisimke. Anasema Abdul Qahirul Baghdad: "Amedai Hisham bin Al-Hakam kwamba Mola wake ana umbo lenye mpaka na mwisho, na kwamba huyo Mungu ni mrefu, mpana, na urefu wake ni kama upana wake…."

Na anasema: Kwamba Ibnu Hisham bin Salim Al-Jawaliqi amepetuka mpaka katika kusema kuwa Mungu ana umbo na kumshabihisha Mungu kwa kuwa amedai kuwa Mungu wake ana sura za kibinaadamu na ana viungo vitano vyenye hisia kama vya binadamu.

Vile vile Ametaja kwamba, Yunus bin Abdur rahman Al-Qummi ni mwenye kupetuka mpaka katika mlango wa tashbihi pia, na akazitaja baadhi ya kauli zake juu ya hilo. Na amesema Ibnu Hazm: "Amesema Hisham kwamba Mungu wake ana shubiri saba kama zake yeye."

Amesema katika pambizo ya kitabu chake: "Tazama vitabu vifuatavyo:
1. Iitiqaadatu firaqil muslimiina wal mushrikiana Uk. 97.
2. A'ayaanus shia: Muhsin Al Amin Juz. 1 UK. 10.
3. Minhaju sunna Juz. 1 Uk. 20.
4. Maqalatu iaslamiyyina Juz. 1 Uk. 106-109.
5. Katika upekuzi wa pili
6. Al-firaqu baynal firaq Uk. 65
7. Rejea iliyopita Uk. 68-69
8. Rejea iliyopita Uk. 70

9. Al-Faslu Juz. 5 Uk. 40

**Maswali**

**1**. Al-Qaffari ameahidi kuwa atatoa nassi kutoka kwenye rejea za vitabu vya Shia, mbona basi hakunukuu hata moja kutoka humo?

**2.** Nini hukumu ya Sheikh asemaye uongo? Rejea moja aliyonukuu ya Shia ni kitabu Aa'yaani shia' cha Seyyid Muhsin Al-Amin na tulipoipitia tukaikuta hata haihusiani na maudhui hayo kamwe!

**3.** Nini hukumu ya sheikh anayedanganya? Anasema: "Amesema Razi,' inafikiriwa kuwa ni Fakhru Razi yule maarufu kwani hiyo ndiyo fikra inayokuja haraka akilini kwa jina la Razi, je unamjua ni Razi yupi ambaye ameyanukuu maneno yake ya kuwatuhumu Shia?

**4.** Nini tofauti ya Tawhid yenu na ile mliyoinasibisha na Hisham bin Al-Hakam na wanafunzi wake, juu ya suala la tashbihi na kumpa Mwenyezi Mungu umbo?

*** * * * * * ***

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:29 AM Page 62



# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Ishirini na moja
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:29 AM Page 63



26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi  Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm

Maswali na mishkili elfu EDITED 28 Aug 2008.qxd 7/2/2011 11:29 AM Page 64



55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliy onyooka
72. Kutawasali
73. Liqaa-u-llaah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
79. Imam Mahdi Katika Usunni na Ushia
80. Hukumu ya Kujenga Juu ya Makaburi

# BACK COVER

Madhehebu ya Shia Ithnaasharia imekuwa ikishutumiwa na Waislamu wengine shutuma ambazo hazina msingi wala hazimo katika imani na itikadi zake. Shutuma hizi zimekuwa zikirudiwa mara kwa mara licha ya kutolewa majibu madhubuti na yakinifu na wanavyuoni wa zamani na wa sasa.

Kutokana na kasumba hii, mwandishi wa kitabu hiki ameamua kukusanya maswali na mishkili elfu moja kutoka kwenye vitabu vya Kisunni na kutoa hoja kabambe kuzijibu shutuma hizo wanazozuliwa wafuasi wa madhehebu ya Shia. Katika kulitekeleza jukumu hili, mwandishi ametegemea rejea zao za msingi kutoka katika (vitabu vya) hadithi, tafsiri, fikihi na itikadi, na kauli za viongozi wao wakubwa kuanzia wa zamani hadi wa sasa.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
**Al-Itrah Foundation**
S.L.P. - 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info